# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumamosi Januari 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581554

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




**HERNÁNDEZ: TUTAITAWALA REAL KESHO**

UKURASA 21

# Sherehe miaka 60 Mapinduzi zafana

• **Viongozi** kimataifa, wastaafu washiriki, gwaride, zana za kivita vyanogesha... *Endelea ukurasa 2*




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwapungia mkono wananchi wakati akiwasili katika Uwanja wa Amani, jijini Zanzibar jana, wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**ZIARA YA BITEKO YALETA MATOKEO CHANYA MTWARA**

ZIARA ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko...

UKURASA WA 5

**OFISI YA WAKILI MKUU YAANZA MFUMO WA MASHAURI KIDIJITALI**

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imeanza kutumia mfumo wa...




UKURASA WA 22

**NIMEREJEA NYUMBANI - SANCHO**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United...

## Meneja TANROADS afariki dunia akiwa mbio za marathon

UKURASA 2

UKURASA WA 3

**Mwili** mwanamke aliyesombwa na maji wapatikana

UKURASA WA 4

**Mbolea** ya ruzuku yawatia matatani viongozi AMCOS



UKURASA WA 5

**Baba** adaiwa kuua kichanga kwa kipigo

## Maafa ya mvua yatikisa kila kona

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA, MLANDEGE FAINALI YA KIUMENI** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na viongozi mbalimbali waliohudhuria sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Uwanja wa Amani jana. **PICHA: IKULU**

# Sherehe miaka 60 Mapinduzi zafana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHAMRASHAMRA za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizofanyika uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar zilifana, kutokana na shughuli mbalimbali huku wananchi kutoka mikoa mitano ya Unguja na Pemba wakiujaza uwanja huo.

Majukwaa yote ya uwanja huo yalijaa watu huku rangi za njano na kijani ambazo ni maalum kwa maadhimisho hayo zikihanikiza sherehe hizo.

Licha ya joto kali, wananchi hawakujali badala yake waliendelea kucheza kwa vifijo kwa nderemo wakifurahia siku hiyo maalum ambayo Zanzibar ilikombolewa kutoka katika makucha ya ukoloni.

Aidha, ulinzi na usalama uliimarishwa ndani na nje ya uwanja huku baadhi ya barabara zinazoelekea katika uwanja huo zikifungwa kwa muda.

Milango ya uwanja huo ilifunguliwa majira ya saa 4:00 asubuhi ili kutoa nafasi kwa wananchi kuingia pamoja na viongozi walioko madarakani, wastaafu na viongozi wa mataifa mbalimbali na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania.

Viongozi wa mataifa ya kigeni waliohudhuria sherehe hizo ni pamoja na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni na Paul Kagame wa Rwanda. Wengine ni Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua na Waziri Mkuu wa Burundi, Gervais Ndirakobuca.

Kabla ya viongozi hao wa kigeni kuwasili, walianza viongozi wa kitaifa wakiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sherehe na Mapambo akifuatiwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman na baadaye Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifuatiwa na Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango, wakiwa wameongozana na wenza wao.

Viongozi wengine waliohudhuria katika maadhimisho hayo ni Rais mstaafu wa Tanzania, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, mawaziri wakuu wastaafu, majaji wakuu na viongozi wengine wa vyama na serikali.

Kuwasili kwa viongozi hao ilikuwa kama rasharasha lakini uwanja ulilipuka kwa vifijo na nderemo saa 10:00 jioni alipoingia Rais Dk, Samia Suluhu Hassan. Baada ya kuwasili, alipokea salamu ya heshima ya Rais kutoka vikosi vya ulinzi na usalama vilivyopamba gwaride la sherehe hizo.

Hatimaye saa 10:15 jioni, Uwanja wa Kumbukumbu ya Amaan ulilipuka zaidi kwa shangwe na nderemo baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwasili akiwa katika gari la wazi.

Mara baada ya kuwasili, wimbo wa taifa wa Zanzibar, wa Tanzania na wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na wimbo maalum wa ukombozi wa Zanzibar maarufu kama "Sisi Sote Tumegomboka" ziliimbwa. Kumalizika kwa nyimbo hizo kulifuatiwa na mizinga 21 iliyopigwa kisha Rais Mwinyi kupata nafasi ya kukagua gwaride.

Sherehe hizo ambazo ni mara ya kwanza kufanyika nyakati za jioni, zilipambwa pia kwa maandamano ya wananchi na wafanyakazi.

Baadae gwaride lililoundwa na gadi 10 ambazo kila moja ilikuwa na askari 102, lilipita mbele ya Rais kwa mwendo wa pole na kasi kutoa salamu kwa Rais.

**KIKOSI CHA MAKOMANDO**

Ukafika wakati wa Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWT) Kikosi cha Makomando kuonyesha manjonjo yao wakiwa na ndege za kivita zenye uwezo wa kubeba mzigo wenye uwezo wa tani saba.

Pia kulikuwa na maonyeho ya kazi za vikosi vya ulinzi na usalama vikiwa na zana za kivita katika kutekeleza majukumu yao ya kazi sambamba na urushaji wa njiwa na maputo ambayo yalioneshwa na Wazanzibari ambao walizaliwa Januari 12, 1964.

**VIONGOZI WAZUNGUMZA**

Akitoa salamu katika sherehe hizo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, alimshukuru Dk Mwinyi kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana Zanzibar ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake.

"Kwa kweli hatuna cha kukulipa tunasema ahsante sana Mwenyezi Mungu akubariki. Tukushukuru katika kipindi hiki, shughuli ilikuwa ya aina yake," alisema.

Rais Museveni aliwapongeza wananchi wa Tanzania kwa kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ambayo ndiyo yaliyowapatia uhuru Wazanzibari.

Alisema serikali ya awamu ya kwanza ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mzee Abeid Amani Karume, ilikuwa na fikra kama za viongozi wengine wa Afrika za kutaka kungana kwa ajili ya kuleta maendeleo barani Afrika.

Museveni alisema maendeleo ya Afrika yataletwa na waafrika wenyewe hivyo ni muhimu kufanya biashara pamoja na kushikamana kwenye taasisi za kikanda ikiwamo Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aliipongeza Zanzibar na Tanganyika kwa kuungana na kuulinda Muungano wa Tanzania ambao umekuwa nguzo muhimu huku akiwashangaa wale wanasiounga mkono na kuwafananisha na vipofu na ni sawa na wanyonyaji.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, aliwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kudumisha malengo ya Mapinduzi na kutekeleza matarajio ya waasisi wa mapinduzi hayo.

Alisema mapinduzi ya Zanzibar ndiyo yaliyoondoa unyanyasaji, kuwapa uhuru wananchi wa kujiamulia mambo yao na kwamba ndiyo yaliyofanikisha kuwapo kwa Muungano wa Tanzania.

Alisema hakuna kisichowezekana kama watu watashirikiana na kwamba Muungano wa Tanzania umeonyesha kuwa Waafrika wanaweza.

Naibu Rais wa Kenya, Gachagua, akimwakilisha Rais William Ruto, alisema Kenya itaendelea kushirikiana na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwenye sekta mbalimbali na kwamba maendeleo katika Afrika Mashariki yatapatikana kwa kushirikiana kiuchumi.

Ndirakobuca akiwasilisha salamu za Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye, alisema furaha ya Wazanzibari kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ni ya wananchi wa Burundi pia na kupongeza hatua kubwa zilizofikiwa kwenye maadhimisho hayo.

Rais Samia alisema Wazanzibari wana kila sababu ya kujipongeza kwa kutimiza miaka 60 wakiwa katika safari nzuri ya mendeleo, ambayo ndio imeanza kutengeneza mazingira mazuri ya kimaendeleo.

Rais Mwinyi aliwashukuru viongozi wote wa kitaifa na wa nje ya nchi pamoja na wananchi wote waliohudhuria madhimisho hayo na kufanikisha harakati zote zilizoanza tangu Desemba 20, mwaka jana.

"Mungu ayadumishe Mapinduzi haya ambayo yanatimiza miaka 60 kwa mafanikio makubwa," alihitimisha Dk. Mwinyi.

# Meneja wa TANROADS afariki kwenye marathon

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Mlima Ngaile, amefariki dunia wakati akishiriki mbio za Wiloles Foundation Marathon 2024.

Mbio hizo zilizofanyika jana asubuhi, zinalenga kuchangia matibabu ya watoto waliozaliwa kabla ya muda wao (njiti) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Ruvuma ya Songea (HOMSO).

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Wiliam Kapenjama, alisema tukio hilo lilitokea jana saa 3:00 asubuhi katika eneo la barabara karibu na baa ya Shefazi, Kata ya Matarawe, Manispaa ya Songea.

Alisema walifika asubuhi katika eneo la viwanja vya michezo vya Majimaji ambako walijisajili kisha wakaanza kukimbia umbali wa kilometa tano.

Kapenjama alisema kundi hilo aliliongoza na kabla hawajamaliza kilometa hizo, wakiwa mlimani, Mhandisi Ngaile aliwapita wenzake kwa kasi eneo hilo na haikuchukua muda ndipo alipoanguka.

Alisema jitihada za kumpatia matibabu ya huduma ya kwanza zilifanyika kisha alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa matibabu zaidi.

"Ni kweli tukio limetukuta tukiwa katika mbio maarufu za Wiloles Foundation Marathon ambako tulikuwa tumeanza pamoja kukimbia.

"Tulipofika maeneo ya barabara karibu na baa ya Shefazi, mwenzetu alitupita kwa kasi na baadaye alianguka na kukimbizwa hospitalini ambako ilielezwa alipofikishwa chumba cha huduma za dharura, tayari alikuwa ameshafariki dunia akiwa mjini," alisema.

Kapenjama alisema tayari amewasiliana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, kwa ajili ya taratibu zingine, ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na mwajiri wake kwa taratibu zaidi za mazishi.

Mwenyekiti wa Wiloles Foundation Marathon, Yusuph Mwikoki, alisema maandalizi ya mbio hizo yalikuwa vizuri kwa zaidi ya mwezi mmoja na jana asubuhi ndipo zilianza.

Alisema mbio hizo ziliwashilikisha watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali na taasisi mbalimbali na pamoja na wa vyama vya siasa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Marko Chilya, alipohojiwa kwa njia ya simu, alisema tayari Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wataalam wengine wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo chake.

Nipashe haikumpata Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Magafu Majura, ambaye alikuwa mmoja wa washiriki wa mbio hizo na ndiye aliyetoa huduma ya kwanza kwa Mhandisi Ngaile baada ya kuanguka.

HABARI KITAIFA

# Maafa ya mvua yatikisa kila kona

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MVUA inayoendelea kunyesha sehemu mbalimbali nchini, imesababisha maafa kwa ikiwamo vifo na kuharibu miundombinu.

Mbali na uharibifu na maafa hayo, zaidi ya abiria 1,200 wanaosafiri na treni ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam Kwenda Kigoma wamekwama kwa zaidi ya saa 17 katika kituo cha reli cha Morogoro.

Wasafiri hao wamekwama eneo hilo baada ya kipande cha Morogoro na Dodoma kuathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha. Kutokana na kukwama huko, wameiomba serikali kuwasaidia usafiri wa mabasi.

Mmoja wa abiria hao, Amana Dunia, aliiambia Nipashe kuwa walitoka Dar es Salaam juzi asubuhi na kusimamishwa Ruvu saa 3:00 asubuhi wakiambiwa njia ni mbaya na baadaye waliendelea na safari hadi Morogoro.

Dunia alisema walifika kituo cha Morogoro saa moja usiku na kuambiwa kuwa wataondoka saa 3:30 usiku, lakini safari hiyo haijaendelea hadi walipokuwa wanazungumza na Nipashe majira ya mchana.

Abiria hao walisema wana changamoto ya kukosa chakula kutokana na waliko, hivyo wameomba serikali kuwasaidia.

Mwanafunzi wa Kidato cha Pili mkoani Kigoma, Hawa Bakari, aliomba serikali kuharakisha usafiri wa mabasi na kuwapa kipaumbele wanafunzi kusafiri kwanza kwa sababu wanamaliza fedha za matumizi kwa ajili ya chakula njiani.

Mfanyabiashara mkoani Kigoma, Juma Mgunda, aliomba serikali kuweka utaratibu wa kufanyia marekebisho maeneo korofi wakati wa kiangazi badala ya kusubiri masika na kufanya wasafiri kutumia muda na siku nyingi njiani.

"Hali hii hujitokeza mara nyingi nyakati za mvua Miundombinu ya reli huharibika tena katika maeneo maarufu kabisa na TRC (Shirika la Reli Tanznaia) hawashtuki kutengeneza mapema," alihoji.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Mkuu wa Kituo cha Reli Morogoro, Herman Ngonyani, alisema tayari wameshaandaa utaratibu wa kuwasafirisha abiria hao kwa mabasi ikiwa ni pamoja na kuwapatia huduma za msingi.

Ngonyani alisema abiria hao watasafirishwa kwa mabasi kwa kuyatumia yatakayoleta abiria wengine waliokwama na treni katika reli mkoani Dodoma iliyokuwa inakwenda Dar es Salaam.

Alisema abiria hao watasafirishwa kwenda Morogoro na baadaye Dar es Salaam kwa kutumia treni iliyopo.

Mabasi hayo yatakayoleta abiria wanaokwenda Dar es Salaam, alisema yatasafirisha abiria wanaokwenda mikoa ya kati hadi Dodoma ambako huko watachukuliwa na treni hadi wanakokwenda.

Ngonyani alisema awali waliandaa taratibu za kufanya ukarabati wa miundombinu ya madaraja yaliyosombwa na maji kwenye maeneo kadhaa ya Mazimbu mkoani hapa yaliyokwamisha usafiri huo.

Alisema mvua zilizoendelea kunyesha usiku wa kuamkia Januari 10, mwaka huu, zilisababisha uharibifu wa madaraja katika maeneo ya Mkata kwenye kituo cha kati, hivyo kuanza kufanyiwa ukarabati uliokamilika asubuhi.

Ngonyani alisema serikali ina utaratibu wa kulipia gharama za wasafiri pindi wanapokwama njiani kupitia njia ya reli, watawalipa kupitia taarifa zao za usafiri hata watakapokuwa wameshafika wanakokwenda.

Alisema treni hiyo ya abiria aina ya Dilux ilianza safari zake jijini Dar es Salaam juzi majira ya saa 3 asubuhi na kukwama kwenye vituo vya Pugu, Ruvu na baadaye Morogoro na ilifika kituoni hapo majira ya saa 1:45 usiku.

Hadi sasa treni tatu za abiria zimekwama katika vituo vitatu vilivyopo nchini kikiwamo kituo cha Dodoma-Singida, kituo cha Manyoni na Morogoro kutokana na mvua zanazoendelea kunyesha.

## Mwili uliosombwa na maji wapatikana

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MWILI wa Mwanahamisi Issa (35), mkazi wa kata ya Bigwa, Manispaa ya Morogoro, mmoja wa wanafamilia wanne waliosombwa na maji ya mafuriko, umepatikana katika bwawa dogo pembeni mwa Mto Mgolole.

Mwanahamisi ni mmoja wa wanafamilia waliosombwa na maji Jumatano mkoani hapa baada ya mvua kubwa kunyesha na wao kuamua kujiokoa kwa kuvuka mto huo ambao hawakufanikiwa.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Mrakibu Shabani Marugujo, alisema mwili huo umeonekana katika bwawa lililojitengeneza lenyewe kutokana na mvua kubwa zinazonyesha.

Alisema umepatikana kilometa 1.2 kutoka eneo alilozama baada ya kusombwa na maji kwenye Mtaa wa Lukuyu ulioko kwenye kata hiyo.

Wakazi wa kata hiyo, akiwamo Jemima Mkude, walishukuru serikali kwa jitihada zao na kuhakikisha mwili huo unapatikana licha ya kutoonekana kwa siku tatu mfululizo.

Mmoja wa wanafamilia wa marehemu hao, Jovin Lawi, alishukuru serikali kupatikana kwa mwili wa shangazi yake ambapo maziko yake yalifanyika jana katika makaburi ya Kola walikozikwa marehemu walioopolewa awali.

Akizungumza kwenye maziko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebecca Nsemwa, aliitaka jamii kuwa makini na mvua zinazoendelea kunyesha ikiwamo kuhama katika maeneo hatarishi.

Alisema ni vyema kila mtu akawa mlinzi wa mwenzie kwa kuhakikisha wanajilinda na hawakutwi na maafa ya mafuriko tena, kwa kuzingatia elimu ya uhifadhi wa mazingira.

Waliofariki dunia ni pamoja na bibi Teresia Adolph (73), mjukuu anayeitwa Asnati Thomas (6) na Mwanahamisi ambapo baba wa familia hiyo, Sengo Hamisi (47), alijiokoa kwa kupanda juu ya mti.




Mdau wa Maendeleo mkoa wa Arusha, Nathan Kimaro (wapili kushoto), akikabidhi runinga kwa Mkuu wa Polisi wilaya ya Arusha, SSP George Malema juzi, kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa matukio ya usalama kupitia kamera za CCTV zilizowekwa barabarani mkoani humo. Kushoto ni Mwenyekiti CCM wilaya ya Arusha, Wilfred Soillel. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## ...Watoto watatu wafa kwa kuangukiwa na ukuta

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATOTO watatu wa familia mbili ambao ni ndugu, wamefariki dunia baada ya kuangukiwa na ukuta wa nyumba katika Mtaa wa Zongomela, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Watoto hao waliokumbwa na maafa hayo ni Shija Mihayo (5), Matha Shabani (7) na Maguzu Shija (5).

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:00 jioni baada ya nyumba waliyokuwemo ya matofali ya tope wakijikinga na mvua, kulowa maji na ukuta kuanguka kisha kuwaponda na kusababisha vifo huku mmoja akijeruihiwa.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, alisema katika nyumba hiyo kulikuwa na watoto wanne, watoto watatu ndio waliopoteza maisha na mmoja kujeruhiwa.

Alisema mtoto huyo mmoja ambaye ni majeruhi, alimpeleka yeye mwenyewe Hospitali ya Manispaa ya Kahama kupata matibabu baada ya kufika eneo la tukio kwa sababu alikuwa wilayani Kahama kikazi.

"Wale Watoto wengine watatu ambao awalifariki dunia, walikuwa tayari wananchi wamewakimbiza hospitali. Mimi nilikuwa kikazi wilayani Kahama. wakati napita kwenye mtaa huo, wananchi wakanisimamisha kuomba msaada wa kumbeba mtoto mmoja ambaye ni majeruhi, Salma Shabani miaka 4 ili kumpeleka hospitali ya Manispaa ya Kahama kupata matibabu ndipo nikapewa taarifa ya tukio hilo, "alisema Magomi.

Aliongeza kuwa alipofika hospitalini na kutaka kuwaona watoto wale wengine watatu ambao wananchi waliwapeleka, aliambowa tayari wamehafariki dunia.

Aidha, Kamanda alitoa wito kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kulinda watoto wao na kuacha kukaa katika maeneo hatarishi katika msimu huu wa mvua, ikiwamo mabondeni na mikondo ya maji ili kuepuka kupata madhara na hata kusababisha vifo.

# Viongozi AMCOS matatani mbolea ya ruzuku

**Na Moses Ng'wat,**
SONGWE

VIONGOZI wa Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa, kwa tuhuma za kujipatia mbolea ya ruzuku kwa njia ya udanganyifu.

Wanadaiwa kuuza mifuko 8,738 ya mbolea hiyo kwa wakulima kwa bei ya kulangua kinyume cha mpango wa serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, aliyasema hayo jana ikiwa ni mwendelezo wa operesheni ya kikosi kazi alichounda kwa lengo la kufuatilia mwenendo wa utoaji ruzuku ya mbolea kupitia mfumo wa kidijitali na kuisambaza kwa wakulima kwa bei elekezi ya serikali.

Dk. Michael alimtaja mtuhumiwa wa kwanza kuwa ni Omary Hashimu, ambaye anahusishwa na watuhumiwa wengine watatu ambao ni wafanyabiashara waliokamatwa awali na baadhi yao kufikishwa mahakamani kwa kujipatia mifuko 74,000 ya mbolea kinyume cha utaratibu na kuiuza nje ya mfumo wa serikali.

Alimtaja mwingine kuwa ni Rashid Msyaliha, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) cha Ilomba, wilayani Mbozi ambaye alikutwa na mifuko 2,907.

"Mwenyekiti huyu wa AMCOS amebainika na makosa kadhaa, yakiwamo kununua au kutoa mifuko 624 ya mbolea ya ruzuku kwa kutumia namba ya ruzuku bila ridhaa ya bodi na wanachama wa AMCOS na kuiuza kwa bei ya juu," alisema.

Dk. Michael alisema mtuhumiwa huyo pia alitumia udanganyifu na kujiandikisha kama mkulima wa kijiji cha Ilomba na kusajili shamba lenye ukubwa wa ekari 1,000 na kujipatia mbolea ya ruzuku mifuko 2,096 na kuiuza nje ya mfumo.

"Kama haitoshi Mwenyekiti huyu wa AMCOS pia alitoa taarifa za uongo kuwa ana shamba lingine la ekari 100 katika kijiji hicho cha Ilomba na kujinufaisha na mifuko mingine ya ziada 187 ya mbolea ya ruzuku na kuiuza nje ya mfumo," alisema.

Dk. Michael alitaja watuhumiwa wengine waliokamatwa kuwa ni viongozi watatu wa Idunda AMCOS iliyoko wilayani Mbozi ambao wamekutwa na makosa mbalimbali yakiwamo ya jinai.

Aliwataja viongozi hao kuwa ni Mwenyekiti wa AMCOS hiyo, Yisega Mwazembe, Bahati Mwazembe, pamoja na Sikuzan Mwashwa ambaye ni mhasibu wa kikundi.

"Viongozi hawa wa Idunda AMCOS tuhuma zao ni kununua na kutoa mifuko 5,831 ya mbolea kwa kutumia namba ya ruzuku ya AMCOS bila ridhaa ya bodi na wanachama na mifuko hiyo haikuwafikia wakulima, haikujulikana ilipelekwa wapi?" alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema katika ufuatiliaji zaidi kikosi kazi hicho kilibaini kuwa, namba hiyo ya usajili ya AMCOS hiyo ilitumia jina la Mwenyekiti wake ambapo ni kosa la jinai.

Pia alisema viongozi hao wakidaiwa kutoa taarifa za uongo na kusajili shamba hewa lenye ukubwa wa ekari 1,000.

Dk. Michael alisema watuhumiwa wote watano wanashikiliwa katika Kituo cha Polisi Vwawa, Wilayani Mbozi na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Alisema hadi kufikia sasa kikosi kazi hicho alichokiunda kimekamata mifuko ya mbolea ya ruzuku 100,019 na kwamba operesheni hiyo ni endelevu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Tigo-Zantel Kanda ya Zanzibar, Aziz Said Ali kwenye maonyesho ya biashara ya Zanzibar visiwani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bugando yaingia mkataba kuboresha huduma afya

**Na Halfani Chusi**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Bugando iliyoko Mwanza, imetia saini mkataba wa kuendelea kufanya kazi na kampuni ya (GPITG), kupitia mfumo wake wa eHMS ili kuboresha mifumo ya kielektroniki ya afya.

Mfumo huo unasaidia mambo mengi ikiwamo taarifa za mgonjwa kutoka hospitali moja kuweza kutambuliwa na nyingine, ukusanyaji wa mapato na takwimu ndani ya hospitali pamoja na kuzuia mianya ya ubadhirifu na upigaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Bugando, Dk. Fabian Masaga, aliyasema hayo juzi wakati akitia saini mkataba huo baada ya ule wa awali kutamatika.

"Teknolojia yao ni nzuri na bora, ambayo imekuwa ikitusaidia kuboresha utendaji kazi wetu wa kila siku. Kupitia mfumo wao wa eHMS ambao tumeanza kuutumia siku nyingi na leo (juzi) tunatia saini mkataba mpya kwa ajili kuendelea kuutumia," alisema Masaga.

Mkurugenzi wa Kampuni ya GPITG, Adelard Kiliba, alisema mfumo huo umekuwa ukitumika kwenye hospitali nyingi na umeleta matokeo chanya zikiwamo zile za serikali.

Alisema mfumo huo umetengenezwa kwa kuzingatia vigezo vyote ikiwamo vya wizara ya afya, serikali mtandao, na bima ya afya na kwamba, nia yao ni kuona mifumo wanayoibuni inatoa huduma bora katika vituo vya afya na kuboresha huduma zao, huku akizitaka hospitali nyingine kutumia.

Kiliba alisema unasaidia kuratibu manunuzi, upokeaji, usambaji, uuzaji na matumizi ya dawa na vifaa tiba na kuondoa upotevu wa madawa.

Pia alisema unasaidia kurahisisha uchakataji na utumaji wa madai ya bima kidigitali, usimamizi mzuri wa huduma na watoa huduma ili kuleta ufanisi kwenye utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

"Faida nyingine ni kuwezesha huduma ya afya ya mama na mtoto kuanzia kipindi cha ujauzito mpaka anapojifungua, kusimamia utoaji na upokeaji wa chanjo kwa wagonjwa.

"Unapunguza vifo vinavyotokana na changamoto za utoaji huduma kwa wagonjwa pamoja na kurahisisha upatikanaji na utumaji wa taarifa sahihi za afya kwenda serikalini.

# Ziara ya Biteko yaleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu**

ZIARA ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, aliyoifanya mkoani Mtwara Novemba 14 na 15, mwaka jana, imeleta neema kwa kupeleka mitambo iliyosimama kuanza kuzalisha umeme huku kituo cha Afya Msimbati kikianza kujengwa.

Wananchi Songosongo pia wamepata neema hiyo huku Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, akisema imeleta matokeo chanya kutokana na maagizo yote aliyoyatoa kuanza kufanyiwa kazi ikiwamo mitambo ya umeme ambayo ilikuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu.

Kanali Ahmed alsema hayo juzi wilayani Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi, wakati wa hafla ya uwekaji saini mkataba wa mauziano ya gesi asilia itakayozalishwa katika eneo la Ntorya Kitalu cha Ruvuma kilichoko mkoani Mtwara.

Alisema Dk. Biteko akiwa mkoani Mtwara, alifanya ziara katika kituo cha umeme mkoani humo na kukuta mitambo miwili haifanyi kazi kwa muda mrefu na kuagiza shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuitengeneza na kuanza kuzalisha umeme ili kupunguza changamoto ya upatikanaji huduma hiyo.

Mkuu wa Mkoa alisema kutokana na agizo hilo, mitambo hiyo imefanyiwa ukarabati na sasa inafanya kazi na kuongeza megawati 6.5 kwenye mzunguko.

Aliongeza kuwa ujenzi wa eneo ambalo litawekwa mtambo mwingine wa megawati 20 unaendelea kwa kasi kubwa hali itakayoimarisha hali ya umeme na kuchochea uwekezaji.

"Pia kazi ya ujenzi wa kituo cha kisasa cha afya katika kijiji cha Msimbati inaendelea. Hii yote inatokana na ziara ya Dk. Biteko katika visima vya kuzalisha gesi asilia na mitambo ya kuchakata gesi iliyoko Mnazi Bay, Kata ya Msimbati. Naibu Waziri Mkuu aliagiza wananchi katika eneo hilo wapate huduma bora zikiwamo za afya, barabara na pia kupata gawio la ushuru wa huduma linaloenda kwenye halmashauri.

Kile anachokisisitiza Dk. Biteko ni kuwa miradi inapotekelezwa katika eneo lazima ibadilishe maisha ya wananchi, ikiwamo pia upatikanaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, afya, barabara na maji," alisema.

Katika hatua nyingine, Kanali Ahmed alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati mkoani Mtwara ikiwemo ya afya, miundombinu na nishati na kwamba mradi huo wa gesi asilia wa Kitalu cha Ruvuma unaotekelezwa mkoani Mtwara, wataulinda na kuutunza kwa ajili ya wananchi wa Mtwara na taifa kwa ujumla.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Biteko alieleza kufurahishwa na utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa wakati wa ziara yake ambayo yameanza kutekelezwa ikiwamo wananchi wa songosongo kupatiwa usafiri wa uhakika utakaowawezesha kuvuka maji kwenda wilayani Kilwa na pia kusambaziwa na kupatiwa umeme wa uhakika.

Dk. Biteko alisema hali ya umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara itazidi kuimarika baada ya kuingia pia kwenye gridi ya taifa ya umeme kutokana na laini ya kV 220 inayojengwa kutoka Songea hadi Mtwara - Lindi.

Naibu Waziri Mkuu alisema hiyo inakwenda sambamba na ujenzi wa laini zingine za umeme katika maeneo tofauti ya nchi pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme.

# Wagonjwa 15 hupokewa MNH kwa siku kwa huduma za tiba mazoezi

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili Tawi la Mloganzila, Idara ya Fiziotherapia, hupokea takribani wagonjwa 13 hadi 15 kwa siku, ambao hufanyiwa huduma ya mazoezi maalum wakiwamo waliopata ugonjwa wa kiharusi.

Mfiziotherapia Mwandamizi wa Hospitali hiyo, Patrick Foster, aliyasema hayo juzi akizungumza na Nipashe, akieleza umuhimu wa huduma hiyo kwa wagonjwa hao, ikiwamo kuimarisha viungo vya mwili.

"Kwa kifupi ni huduma ya fiziotherapia, si mazoezi tu kuna mambo mengi, huduma hii ni muhimu sana kwa wagonjwa wa kiharusi kuanzia wakati anapopata na kuendelea. Kutembea na kutumia mikono ni kipaumbele.

"Wengi wanaowahi kupata huduma na kuendelea nayo matokeo ni mazuri. Kuna wanaopona na kuendelea na shughuli zao na kuna wanaobaki na madhara ya 'stroke' (kiharusi). Tunapokea (Mloganzila) wagonjwa wapatao 300 kwa mwezi kupata huduma hii, wakiwamo wenye kiharusi," alisema Foster.

Ashura Kazema, Mfiziotherapia Mbozezi katika Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu kwa Watu Wazima, Kitengo cha Utengamao na Mazoezi kutoka hospitali hiyo, alisema wanaopata huduma hiyo hupata mabadiliko.

"Asilimia tano ya wagonjwa wanaougua kiharusi na kufanya mazoezi, wana uwezekano kurudi katika hali ya kawaida na kuondokana na kukakamaa na mikono na miguu. Baadhi ya viungo vya mwili hasa miguu na mikono, kwa wagonjwa hawa kukakamaa hivyo inahitajika mazoezi ya viungo hivyo, ili warejee kwenye hali yao ya awali.

"Huduma huenda kwa awamu hapa hospitalini, lakini pia mgonjwa anaweza kuendelea kufanya mazoezi akiwa nyumbani kwa msaada wa mtu na baadae akafanya mazoezi mwenyewe," alisema Kazena.

Wiki hii, hospitali hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kiharusi Duniani (The World Stroke Organization), ilizindua mafunzo maalumu kwa wataalamu wanaoshughulikia magonjwa ya kiharusi, ili kuboresha huduma kwa wagonjwa hao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Hospitali hiyo na Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Nje (OPD), Dk. Elimeena Meda, alisema mafunzo hayo ni muhimu kuokana na ongezeko la wagonjwa wa kiharusi.

"Ni muhimu watoa huduma wote kujua namna bora ya kuwahudumia wagonjwa hao. Tumeona sababu ya kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa kiharusi.

"Mafunzo haya yanahusu kada zote zinazoshiriki katika mnyororo wa kuwahudumia wagonjwa wa kiharusi, ili kuboresha huduma wanapokuwa hospitalini hadi wanaporuhusiwa" alisema Dk. Meda.

Mwandaaji wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Sarah Matuja, alisema kwamba ugonjwa wa kiharusi umekuwa tishio nchini na unawakumba watu wenye umri kati ya miaka 40 hadi 60 na hivyo kuathiri nguvu kazi ya jamii.

Mafunzo hayo yameanza kutolewa na wataalamu bingwa wa magonjwa ya kiharusi duniani kuanzia Januari 9 hadi Machi 19, mwaka huu, yanahusisha wakufunzi ambao ni Madaktari Bingwa wa Kiharusi Duniani, yakiwa ya nadharia na vitendo.

# Baba adaiwa kuua kichanga kwa kipigo

**Na Vitus Audax**

MTOTO mwenye umri wa miezi mitano, Leonard Kubilu, anadaiwa kupigwa hadi kuuawa na baba yake mzazi, Kubilu Mayege (20), ambaye ni Mchimbaji mdogo wa madini na Mkazi wa Mtaa wa Kilimahewa, Mamlaka ya Mji Mdogo Katoro mkoani geita.

Mayege anadaiwa kufanya kitendo hicho kwa kile kinachodaiwa ni kutokana na mtoto huyo kulia wakati wa usiku.

Baba huyo, anadaiwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili mtoto huyo kwa kutumia mkanda wa suruali na kiatu na kisha kumrusha kwenye kochi, hali iliyosababisha jeraha kichwani na kumsababishia kifo.

Mzazi huyo anadaiwa kufikia hatua hiyo baada ya kukasirishwa na kitendo cha mtoto huyo kulia nyakati za usiku alipombembeleza bila kukoma, hivyo kumshushia kipigo pamoja na mama wa mtoto huyo.

Akisimulia tukio hilo, mama mzazi wa mtoto, Riziki Leonard, alisema baba huyo alifika majira ya 5:00 usiku akampakulia chakula na baada ya kula, alikwenda kulala na kukuta mtoto analia, hivyo kuanza kumbembeleza huku akimpiga makofi.

"Baada ya mtoto kuendelea kulia, alianza kumpiga makofi ya nguvu kisha kumrusha kwenye kochi ambapo tuliona amelegea lakini alimfuata pale na kuanza kumpiga kwa kiatu na mkanda akisema nitakuua, nitakuua, nikamzuia lakini hakusikia," alisema.

Riziki aliongeza kuwa baada ya mtoto kutulia na kulegea kwenye kochi, alikwenda kumzuia lakini baba huyo hakusikia akaendelea kumpiga mikanda pamoja na mama yake ambaye pia ilimng'ata shavu la mama huyo.

Baada ya kutekeleza unyama huo, alisema mwanamume huyo alitokomea kusikojulikana hivyo kumlazimu kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa kitongoji.

Akithibitisha tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kilimahewa, Michael Chuma, alisema alipokea taarifa kutoka kwa mwenyekiti wa kitongoji majira ya saa 7:00 usiku, hivyo kufika katika eneo la tukio na kukuta mtoto huyo akiwa tayari amefariki dunia.

Chuma alisema baada ya kubaini hivyo alitoa taarifa polisi waliofika na kuchukua mwili huo kuupeleka hospitalini kwa ajili ya vipimo zaidi huku hatua za kumtafuta mtuhumiwa zikiendelea.

"Tulibaini kuwa tayari mtuhumiwa amekimbilia kusikojulikana, hivyo Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Chuma.

Ndugu wa Marehemu, Emannuel Sospeter, alisema baada ya kufika hospitalini mwili ulifanyiwa uchunguzi na kubainika kuwa mtoto huyo alipata maumivu makali katika maeneo ya kichwa na jeraha la ndani hali iliyosababisha damu kuvuja kwa ndani na kumsababishia kifo.




Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara (kulia), akizungumza jambo kwenye Banda la Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), alipoambatana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Ali Possi (kushoto kwake), walipotembelea Banda la TCAA kwenye Maonyesho ya Maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yanayofanyika katika viwanja vya Fumba, Zanzibar na kupokelewa na Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka ya TCAA, Teophory Mbilinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ofisi ya Wakili Mkuu yaanza mfumo wa mashauri kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imeanza kutumia mfumo wa mashauri wa mahakama wa kielektroniki ili kuongeza matumizi ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA).

Mfumo huo pia utaongeza uwazi, uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa kwa haraka na imani kwa wananchi kuhusu utendaji kazi wa vyombo vinavyotoa haki kwa wananchi.

Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo elekezi kuhusu Mfumo wa Kielektroniki wa Mashauri ya Mahakama Kuu ya Tanzania (e-CMS) na utunzaji wa nyaraka za serikali mjini Morogoro.

Alisema OWMS imeona ni muhimu kwa watumishi kupata mafunzo kuhusu e-CMS ili kuutumia kwa pamoja na kusomana na mfumo wa usajili wa mashauri wa OWMS (CIMS) kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, kuongeza tija na ufanisi katika usajili, matumizi na uendeshaji wa mashauri baina ya Mahakama, OWMS, wadau na wananchi.

Mulwamba alisema e-CMS imefanikisha utoaji wa taarifa kwa wahusika wa shauri kuwa limesajiliwa na kupangiwa jaji au hakimu na kutoa mwanya wa kujumuisha taarifa za taasisi zingine za serikali ili kutumika na kusomana.

Pia alisema mfumo huo utaendana na taratibu za utendaji wa Mahakama; Majaji kuandika mwenendo wa mashauri kwenye mfumo badala ya majalada; kupanga mashauri kwa kila jaji badala ya jaji mmoja kuwa na mashauri mengi au machache.

Pia alisema mfumo wa e-CMS umefanikisha usajili wa namba ya utambuzi wa kesi ambayo haijirudii na kutumiwa na mahakama nyingine na kusajili taarifa za mashauri ya Mahakama ya Rufani wakati awali haikuwepo.

Mfumo huu pia umesaidia kutambia na kuruhusu matumizi ya taarifa kutoka NIDA (mamlaka ya VitAmbulisho vya Taifa), BRELA (Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara) Chama cha Mawakili wa Tanganyika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na taarifa za taasisi nyingine. Pia umetambua na kubaini usajili wa Mawakili na Waendesha Mashtaka halali kwa kuwatambua kwa namba zao na si vinginevyo," alisema.

Mulwambo alipongeza Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kujenga mfumo wa e-CMS kwa kuwa haki itapatikana kwa wakati kwa watu wote bila kujali mahali alipo kwa kutumia TEHAMA na kwa kuzingatia kuwa OWMS ni mdau muhimu, hivyo mafunzo kuhusu mfumo huo yanatolewa kwa washiriki 27 kutoka OWMS na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwawezesha watumishi kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya usajili wa mashauri, utunzaji wa kumbukumbu za kielektroniki na namna nzuri ya kuwahudumia wateja wa ndani na nje.

Aidha, aliwataka washiriki hao kuzingatia mafunzo hayo ili waweze kutumia ujuzi watakaoupata na kuyafanyia kazi kwa kuzingatia uadilifu na usiri katika utendaji kazi kwa kuwa Masjala ya Sheria ni Ofisi nyeti katika kutunza nyaraka za serikali.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masjala ya Sheria OWMS, Dennice Leonard, alisema e-CMS itawawezesha wananchi kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa mashauri Mahakamani kwa kupata ujumbe kwenye simu zao za mkononi na barua pepe.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Taifa Stars katika fainali za AFCON

**FAINALI** za Kombe la Mataifa ya Afrika maarufu kwa jina la AFCON zinatarajiwa kufanyika kuanzia leo na kumalizika ifikapo Februari 11, mwaka huu huko nchini Ivory Coast.

Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), ni moja kati ya mataifa yaliyofuzu kushiriki fainali hizo, ikiwa imepangwa katika Kundi F.

Taifa Stars itaanza kurusha karata yake katika fainali hizo Januari 17 kwa kucheza dhidi ya Waarabu wa Morocco halafu itakutana na Zambia Januari 21 na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi kwa kukutana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), hapo Januari 24, mwaka huu.

Hii ni mara ya tatu kwa Taifa Stars kushiriki fainali za mashindano hayo makubwa katika ngazi ya timu ya taifa, lakini mara mbili ikishindwa kuvuna hata pointi moja.

Katika kujiandaa na fainali hizo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche, kwa kushirikiana na Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), iliwasaka wachezaji wenye asili ya Tanzania wanaocheza Ulaya ili kuwaita na kukiongezea nguvu kikosi.

Ubora na mabadiliko ya Stars ulionekana katika mechi ya mwisho ya kusaka tiketi ya AFCON, ilipocheza ugenini dhidi ya Algeria ambapo dakika 90 zilipomalizika, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana, Tanzania ikapata pointi moja muhimu iliyowapeleka katika fainali za mwaka huu, ambazo zinatambulika kama ni michuano ya mwaka uliopita.

Hilo liliwezekana na katika mechi tatu za mwisho za kusaka tiketi ya kucheza AFCON, kwa mara ya kwanza wadau wa soka wa Tanzania walishuhudia sura mpya za wachezaji na hii iliongeza hamasa na ushindani wa namba kwenye kikosi cha Stars.

Kuelekea mashindano hayo, Amrouche amekaririwa akisema kikosi chake kimeimarika na kinaweza kupata matokeo chanya kama itatumia vyema nafasi watakazopata au makosa yatakayofanywa na wapinzani wao kwa sababu mpira wa miguu ni mchezo wa makosa.

Tunapenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha wachezaji wote watakaopata nafasi ya kucheza kuongeza umakini na utulivu katika kutekeleza majukumu, kila mchezaji anatakiwa kufahamu majukumu ya nafasi anayoicheza, kila mchezaji anatakiwa akumbuke wanakutana na wachezaji wenye uzoefu wa kushiriki mashindano mbalimbali makubwa, hivyo hawatakiwi kuwapa nafasi ya kutawala mchezo.

Mbali na kuipa heshima Tanzania, mashindano hayo ni sehemu muhimu kwa kila mchezaji kujiongezea thamani na vile vile kujitangaza kwa makocha na mawakala ambao watakuwa wanafuatilia kila mechi ili kupata nyota wa kuwasajili katika klabu zao zinazoshiriki ligi nyingine zilizoendelea huko Ulaya.

Lakini pia tukumbuke kuanza kwa fainali hizi, ndio maandalizi ya kuelekea fainali zijazo, hivyo wachezaji vijana ambao hawakuitwa katika kikosi kilichoko Ivory Coast, watumie muda huu kujifunza ili kukuza viwango vyao tayari kuisaidia nchi na timu zao katika mashindano yanayokuja.


Lakini bila kuwasahau wadau wa soka, huu ni wakati muhimu wa kuungana na kuiombea Taifa Stars ifanye vizuri katika mashindano haya na kuweka tofauti zetu pembeni, tuhamishie mahaba tuliyokuwa nayo kwa klabu zetu pendwa kuhamia katika taifa letu.

Mashabiki tunatakiwa tufahamu mipaka yetu, tukubali kazi ya kuchagua au kupanga kikosi ni kocha na sisi jukumu letu ni kuiombea timu kupata matokeo chanya na kushangilia.

Tunawakumbusha wachezaji wa Taifa Stars kuingia katika fainali hizo kwa kujiamini na kutowahofia wapinzani wao, wafahamu hata mbuyu ulianza kama mchicha, hivyo wakipambana na kucheza kwa juhudi, kupata mafanikio ni jambo linalowezekana.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

Muungwana Lazima Nilonge

# Kila la heri Stars AFCON, tunahitaji kufanya vyema, hatuhitaji makubwa

**HATIMAYE** pazia la fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) linatarajiwa kufunguliwa leo nchini Ivory Coast wakati timu 24 zilizofuzu zitakapomenyana kusaka mfalme wa mwaka huu.

Kwa sasa linashikiliwa na Senegal iliyoifunga Misri kwa mikwaju ya penalti 4-2 baada ya kutoka suluhu, 2022.

Mwaka huu, timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars nayo imo kwenye kinyang'anyiro hicho ikiwa kwenye kundi F pamoja na timu za Zambia, Morocco, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kila kitu kimeshafanyika, ikiwemo maandalizi, kuchagua wachezaji, michango pamoja na hamasa, kwa hiyo kilichobaki sasa ni uwanjani tu.

Ni Kocha Mkuu Adel Amrouche na wachezaji wake ndiyo wamebaki wanaotazamwa kuona watawaletea nini Watanzania.

Stars itashuka dimbani kucheza michuano hiyo Jumatano ijayo dhidi ya timu ya taifa ya Morocco.

Kwa mara ya kwanza Watanzania wanashiriki michuano hiyo wakiwa na idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Wamesakwa kote walikokuwa, lakini pia serikali inawataka Wabongo wote wanaoishi nje ya nchi na wana uwezo wa soka waungane na wenzao kwa ajili ya kulitetea taifa kwenye nyanja za soka.

Ndiyo maana tunaona kwenye kikosi kuna baadhi ya wachezaji ambao hawajawahi kuonekana, wengine ni mechi zao za kwanza au pili kucheza.

Nilichofurahi kuwa huu ni mwanzo na mlango wa kwenda kule ambako timu za Nigeria, Senegal, Mali, Comeroon zipo.

Timu hizo wala si ajabu kuita timu nzima kutoka bara la Ulaya asiwemo hata mmoja anayecheza soka la kulipwa Afrika, achilia mbali kwenye nchi yao.

Kilichokuwa kikinikera ni baadhi ya watu kulazimisha Simba na Yanga kuwa na wachezaji wengi wa Kitanzania eti kwa ajili ya manufaa ya timu ya taifa.

Hivi sasa taratibu tumeanza kuona kuwa wachezaji wa Stars wala si lazima watoke Simba, Yanga au Azam.

Wanaweza kutoka hata katika klabu mbalimbali za Afrika na bara la Ulaya, bado ikawa Stars tu.

Huko sasa ndiko tunakoelekea, huku pia tukiwa na baadhi ya wachezaji waliochanganya uraia ambapo awali ilikuwa ni ngumu.

Serikali ya Tanzania kwa maslahi mapana ya nchi imeamua kukaa na kutengeneza utaratibu wa wachezaji wa aina hiyo kutumika kwa ajili ya Taifa.

Huu ni mwendelezo wa serikali kuangalia kwa jicho pana sekta ya michezo kwani imeshawahi kutoa hata uraia kwa Kibu Denis ili mradi tu aitumikie Stars na mpaka sasa yupo kwenye kikosi hicho.

Kwangu mimi naona mashabiki wa Stars bado tusiweke matumaini makubwa kwa kikosi hicho, kama vile kutinga hatua ya robo fainali, nusu fainali, fainali au ubingwa.

Kama itatokea kimoja kati ya hicho itakuwa ni 'bonas', lakini ambacho Stars inadaiwa ni ushindi tu katika mechi zake.

Stars haijawahi kushinda mechi yoyote ya fainali za AFCON mara zote mbili ambazo imefanikiwa kuingia.

Mwaka 1980 ikiwa Kundi A, ilimaliza ikiwa imecheza mechi tatu, ikipoteza mbili na sare moja ikishika nafasi ya mwisho, na 2019 ilipotinga kwa mara ya pili ilimaliza ikiwa imepoteza mechi zote tatu ikishika nafasi ya mwisho katika Kundi C.

Timu kama hiyo si rahisi eti kwa mara hii ya tatu kuweza kufanya makubwa zaidi ya kile kinachotakiwa kufanywa.

Stars hatuidai kombe, fainali, nusu, wala robo, Watanzania kwa sasa tunachoidai ni kuvunja rekodi yake yenyewe ya angalau kupata ushindi wowote ule kwenye fainali hizo.

Huo utakuwa ushindi mkubwa kwa Watanzania, na kama itasonga mbele basi furaha itakuwa kubwa zaidi.

Kila la heri, Stars na Watanzania wote kwenye michuano hii ya AFCON.

# Zanzibar yaweka mikakati ya kupunguza utegemezi mafuta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema Wizara ya Nishati inaendelea kufanya kazi ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya gesi unakuwa wa uhakika ili kupunguza utegemezi wa mafuta nchini.

Amesema kutokana na uwapo wa rasilimali ya gesi hiyo inakadiriwa ifikapo mwaka 2050 uagizwaji wa mafuta utashuka kwa asilimia 28.

Dk. Biteko aliyasema hayo juzi visiwani hapa wakati akishuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa mauziano wa gesi asilia itakayozalishwa katika kitalu cha Ruvuma kati ya Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC) na Ndovu Ditrotion.

Pia kulikuwa na utiaji saini hati ya makubaliano kwa ajili ya kuanzisha uhusiano wa kujenga miundombinu ya kusambaza gesi asilia hususan katika miradi midogo ya gesi ya kimiminika.

Dk. Biteko alisema mikakati ya wizara ni kuhakikisha inasimamia sera ya upatikanaji wa nishati safi ambayo itawafikia wateja mbalimbali kwa urahisi na kwa bei nafuu.

"Sisi kama taifa ni vizuri tukaangalia vitu ambavyo tukivifanya vitawaondoa watu kwenye umaskini kwa haraka zaidi," alisema.

Dk. Biteko alisema kwa sasa gesi inayozalishwa nchini asilimia 80 inatumika kuwa chanzo cha kuzalisha umeme, hivyo TPDC imeandaa mkakati ambao gesi nyingi kubaki kwenye umeme, asilimia 38 na 32 iende kwenye matumizi ya viwandani na asilimia 10 kwa ajili ya matumizi ya watu binafsi.

Aidha, Dk. Biteko alisema njia rahisi ya kuifanya gesi hiyo iwafikie watu wengi, ni kuigeuza kuwa kimiminika ili kuisafirisha kwa gari kwa ajili ya matumizi.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Mussa Makame, alisema utaongeza upatikanaji wa gesi asilia na kuongeza uchumi wa nchi.

Alisema kwa sasa jumla ya futi za ujazo bilioni 1.6 zimegunduliwa na kuhakikiwa ambapo kwa mwaka 2024 katika robo ya pili, TPDC kwa kushirikiana na kampuni zilizosaini mikataba hiyo, imepanga kuchimba kisima kipya ili kuongeza kiasi cha gesi kilichozalishwa.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuzalisha kiasi cha futi za ujazo milioni 60 kwa siku hadi kufikia futi milioni 140 katika kipindi cha miaka mitatu ya kwanza.

Aidha, alisema kukamilika kwa mkataba huo kutaendeleza shughuli nyingine kufanyika ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima vya kuzalisha gesi na ujenzi wa miundombinu ya kukusanya gesi kutoka visimani.

Alitaja shughuli nyingine ni miundombinu ya usafirishaji wa awali, pamoja na ujenzi wa bomba la kilomita 34 za kusafirisha gesi kutoka miundombinu ya ukusanyaji gesi kuelekea kwenye kiwanda cha kuchakata gesi kilioko Mtwara.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kubadilisha gesi asilia kuwa kimiminika, alisema ni wa kwanza kufanyika nchini na utaweka historia katika sekta ya nishati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ARA, Majid Al Shandoudi, alisema wamejipanga kufanya kazi ya usambazaji wa nishati ya gesi kwa ufanisi mkubwa kutokana na kuwa na uzoefu wa kimataifa katika kazi hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Ahmed Abas Ahmed, aliahidi kuutunza mradi huo kwa ajili ya wananchi wa Mtwara na taifa kwa ujumla.

Mkataba wa mauziano wa gesi ni wa nne kusainiwa katika upatikanaji wa gesi katika soko la ndani ambapo mradi wa kwanza ulisainiwa mwaka 2011, wa pili mwaka 2007 na wa tatu mwaka 2016.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (wa tatu kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ujenzi ya Afriq, Mhandisi Charles Bilingi (wa pili kulia), wakati akitoa maelezo kuhusu mradi wa Kongani ya kisasa ya viwanda katika eneo la Kikongo Mlandizi, Kibaha, Mkoa wa Pwani juzi. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Ujenzi wa kongani za viwanda washika kasi

**Na Joseph Mwendapole**

UJENZI wa kongani ya viwanda ya KAMAKA Park ambao unatarajiwa kugharimu Sh. trilioni 3.5 Kibaha mkoani Pwani umefikia asilimia 93 ya ujenzi wake na inatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Hayo yalibainika katika ziara ya Waziri wa Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji, aliyembelea kongani hiyo kujionea maendeleo ya ujenzi na changamoto zilizoko ili kwenda kuzifanyia kazi kupitia mawaziri wa kisekta.

Alimpongeza mwekezaji huyo wa ndani kwa kuthubutu na kuwa na utayari wa kuwekeza uwekezaji mkubwa kama huo ambao utakuwa na manufaa makubwa.

Aidha, Dk Kijaji alisema ujenzi wa viwanda na kongani za kutosha nchini utawezesha kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana wa kitanzania.

Kuhusu changamoto za kongani hiyo, Dk. Kijaji alisema zipo ambazo zimeanza kufanyiwa kazi na kuhusu changamoto ya barabara aliahidi kukaa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ili kuangalia namna ya kufanyia kazi changamoto hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema barabara ya kuanzia Makofia -Mlandizi -Mzenga -Vikumburu -Mloka ni muhimu kwani inapitia eneo la uwekezaji na kwenye miradi ya kimkakati.

Kunenge aliomba ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utakapoanza uanzie Mlandizi kwa maslahi mapana ya eneo hilo.

Kuhusu maji, Kunenge alisema alishazungumza na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye aliahidi kufika kwenye kongani hiyo kujionea uhalisia wa tatizo.

Awali, Ofisa Fedha na Masoko wa KAMAKA Co .Ltd, Tumaini Kabengula, alisema kongani hiyo itakapokamilika itatoa ajira 200,000 za muda na ajira 30,000 za kudumu.

"Mradi ulianza kutekelezwa Oktoba 2021 ,kwa awamu ya kwanza kwenye ujenzi wa lango kuu na uzio, kituo cha polisi, jengo la utawala, ofisi na jengo la makazi ya wafanyakazi wa zimamoto, zahanati, kituo cha umeme wa megawatt 54 ,mfumo wa barabara za nje na ndani na umefikia asilimia 93," alisema Kabengula.

# Wazazi wasiopeleka watoto shule kuchukuliwa hatua

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Nyang`ware, Grace Kingalame, ametishia kuwachukulia hatua wazazi au walezi watakaoacha kuwapeleka wanafunzi shuleni.

Kingalame alisema watoto wote wanaostahili kupelekwa shuleni kuanzia darasa la awali, darasa la kwanza mpaka kidato cha kwanza wanatakiwa kuwa shuleni na si vinginevyo.

Alisema serikali imefanya juhudi kubwa ya kuboresha mazingira na kuimarisha miundombinu ya shule, hivyo hakuna sababu ya kuacha kupeleka wanafunzi hao shuleni.

"Kama Mkuu wa Wilaya hii, sitavumilia wala kusita kuchukua hatua kwa mzazi au mlezi yeyote ambaye atasita kumpeleka mtoto shule kwa minajili ya kufanya shughuli mbalimbali ambazo ni kinyume na haki za mtoto. Nitahakikisha ninakwenda sambamba na wale wanaokiuka utaratibu,"alisema Kingalame.

Pia, aliwaomba walimu katika wilaya hiyo kutimiza wajibu wao ili kupaisha sekta ya elimu katika wilaya hiyo.

"Ninaamini walimu nao watatimiza wajibu wao kuhakikisha tunaipaisha Nyang`ware kwenye sekta ya elimu.

"Ninaamini Nyang`aware ya watu walioelimika inawezekana na tutalifanya hili kwa umoja ili kuhakikisha tunaunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha jamii ya Watanzania inaelimika,"alisema Kingalame.

Alisema Rais Samia amefanya kazi kubwa kuhakikisha mtoto wa Kitanzania anapata elimu nzuri na bora katika mazingira mazuri bila kujali mahali alipo.

"Wilaya yetu ni miongoni mwa zilizonufaika pakubwa kutokana na na juhudi hizo kubwa zinazofanywa na Rais za kuhakikisha tunakuwa na mazingira mazuri, miundombinu, na rasilimali watu kwa maana ya walimu," alisema.

# Migogoro ardhi yampeleka Waziri uwandani

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ameingia uwandani kutatua na kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake ya migogoro ya ardhi katika jiji la Dodoma.

Pinda katika ziara yake hiyo juzi, aliambatana na watendaji wa sekta ya ardhi makao makuu ya wizara, ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma na wale wa Jiji la Dodoma katika eneo la Chang'ombe.

Naibu Waziri alianza ziara yake kwa kutembelea eneo la Chang'ombe Mbwanga ambako mwananchi aliyejulikana kwa jina la Dorothy, alibomolewa kimakosa ukuta wa nyumba yake na Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Pinda alielekeza kujengewa ukuta huo.

"Ninyi mnaoishi hapa sura ya ujirani lazima itengenezwe kwa kuepuka migogoro ya ardhi katika maeneo yenu. Mnataka mpaka waziri aje ndiyo atengeneze ujirani?" alihoji.

Pia alitembelea eneo la Chang'ombe Extension ambako mwananchi mmoja, Ramadhani Kisiju, anadai kumiliki kiwanja alichokuwa akilima kwa muda mrefu.

Katika kutafuta suluhu ya eneo hilo, Pinda aliagiza mmiliki wa eneo analodai Kisiju kumiliki, afike ofisini kwake na nyaraka zote za umiliki kwa lengo la kupata mwafaka wa mgogoro huo.

"Kitu kimoja ninachotaka kukusaidia mzee wangu, ngoja tukaangalie hiki kiwanja uhalali wake halafu baadaye tutakupa majibu," alisema.

Uamuzi wa Pinda kutembelea na kukagua maeneo ya mgogoro uwandani unatokana na kuwasilishwa kwa malalamiko ya migogoro ya ardhi kwake huku baadhi yakihusisha watendaji wa sekta ya ardhi.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda (kulia), akikagua ukuta wa mwananchi uliobomolewa kimakosa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma na kujengwa tena katika eneo la Chang'ombe, jijini humo juzi. **PICHA: WANMM**

# Mbunge afichua fedha za Rais zilivyoibadili Msalala

**Na Joseph Mwendapole**

MBUNGE wa Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, Alhaji Idd Kassimu Idd (CCM), ametamba kwamba fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, zimeibeba halmashauri hiyo.

Akizungumza katika kikao cha wadau wa maendeleo kilichoitishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba, Alhaj Idd alisema Rais Samia ameipa halmashauri hiyo fedha nyingi za maendeleo kuliko halmashauri zingine za mkoa huo.

Alisema hatua hiyo imewezesha miradi mingi ya kimkakati kwenye Halamshauri ya Msalala kusimamiwa na kukamilika kwa wakati na kwa kiwango kinachoridhisha.

"Halmashauri ya Msalala ni miongoni mwa halmashauri zilizopokea fedha zote za kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka serikalini na ni halmashauri ya kwanza kupata fedha nyingi mkoani Shinyanga na ndiyo maana imefanya makubwa kwenye miradi yake chini ya usimamizi mzuri wa mkurugenzi wetu," alisema.

Alitaja baadhi ya miradi iliyotekelezwa kupitia fedha hizo kuwa ni ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Isaka, Mwalugulu, Segese, Bulige, Mwanase ambapo zaidi ya shilingi bilioni 2.5 zilitumika kukamilisha vituo hivyo.

"Halmashauri ya Msalala imekamilisha zahanati 24 ambazo sasa zinatoa huduma, hii yote ni jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano tunamshukuru sana Rais Samia," alisema mbunge huyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba, aliwataka wadau walioshiriki kikao hicho kupitia na kurekebisha kasoro zilizopo kwenye mpango huo tangu ulipoanza kutekelezwa miaka mitatu iliyopita, ili uwe na matokeo chanya zaidi.

"Mpango huu ulianza kutumika miaka mitatu iliyopita na sasa tunauishi, hivyo wadau tunayo nafasi nzuri ya kuchangia ili tufike mwaka 2025/2026 tukiwa pamoja na serikali yetu," alisema na kuongeza.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunajua halmashauri inafanya nini kwa sasa na inalenga kufanya nini baadaye, ninaamini mtindo huu utanitasaidia mimi Mkurugenzi na watendaji wenzangu kuona kasoro wakati wa utekelezaji na kuchukua hatua," alisema Katimba.

Miongoni mwa malengo yaliyomo kwenye mpango mkakati huo ni pamoja na kuwezesha wananchi wa Msalala kufanya kilimo cha kibiashara, uchimbaji wenye faida, kuweka mazingira rafiki kwa wajasiriamali, halmashauri kutangaza fursa za uwekezaji pia utunzaji wa mazingira na afya za wananchi.

Baadhi ya wadau wa maendeleo waliitaka halmashauri hiyo kuboresha zaidi mazingira ya wawekezaji ili kuinua wananchi kwa kuwa, ina mazingira mazuri.

Hakimu Dismas ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Lunguya, alishauri halmashauri kupima maeneo yote yanayomilikiwa na serikali na hasa maeneo ya mahakama kutokana na kuwepo kwa mradi wa kimataifa wa kujenga mahakama.

"Hapa kigezo kikubwa ni ardhi iwe imepimwa, hivyo halmashauri iwezeshe suala hili sambamba na kuwezesha vitendea kazi kwa ofisi za watendaji wa kata/vijiji na kuyajengea uwezo mabaraza ya ardhi ya kata, kwani mabaraza haya yamekuwa yakiingilia shughuli zisizowahusu," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Mibako Mabubu aliwashukuru wadau wa maendeleo ya halmashauri kwa kujitokeza kwa wingi na kutoa maoni yao kuhusu shughuli za halmashauri hiyo.

"Michango mliyoitoa nitahakikisha Mkurugenzi Mtendaji anafanyia kazi yeye na watumishi wote wa halmashauri sanjari na mimi kufanya kazi niliyoagizwa na madiwani," alisema.

# Wanasiasa waonywa kufanya siasa misibani

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAZEE wa mila, viongozi wa kidini na wananchi wanaoishi vijiji vya mipakani katika Tarafa ya Inchugu, wilayani Tarime, mkoani Mara, wamewaomba viongozi wa vyama vya siasa na wanachama wao, kuacha kutumia misiba kulumbana kisiasa.

Wamesema vitendo hivyo vinaashiria vurugu na kutoweka kwa amani msibani na kuwataka wahusika kutumia majukwaa ya kisiasa kupeleka ujumbe wanaotaka na si katika misiba.

Kiongozi wa wazee wa mila, Wangubo Mtongori na mwananchi Sinda Chacha, walisema kuwa, vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wanasiasa kuanza kulumbana katika misiba ya watu wengine kila upande ukidai aliyefariki ni mwanachama wao,vinaleta uvunjifu wa amani.

Mtongori aliomba vitendo hivyo vikemewe kwa kuwa, muda wa kampeni haujafika na hata ungefika, vinapaswa kutendeka katika majukwaa ya kisiasa na si msibani.

Charles Mwita, Mchungaji wa Kanisa la Pentekoste, Mchungaji John Marwa wa Kanisa la EAGT na wananchi Lameck Sinda Chacha , Jumanne Getari na Gimase Marwa pamoja na madiwani walionyesha kusikitishwa na vitendo hivyo wakati wakizungumza kwa nyakati tofauti.

Walisema, "Tunasikitishwa na vitendo vinavyoendelea kufanyika katika matukio ya misiba ya wananchi wanaofariki dunia viongozi wa kisiasa wanapopewa nafasi ya kutoa salamu za rambirambi hutumia nafasi hiyo kutoa maeneo ya kulumbana na chama kingine.

Walisema vitendo hivyo vinahatarisha amani na kuashiria vurugu katika mazishi ya watu wengine ambao hawahusiki wakiwamo wanafamilia waliopata msiba ambao wanatakiwa kufarijiwa na kupewa pole.

Diwani Joh Bosko Mbusiro, Nashon Mchuma na wenzake walikiri kushamiri kwa vitendo hivyo hasa katika vijiji vya mipakani hususani Kata ya Sirari.

"Tunakemea malumbano haya ya kisiasa na tunawaomba viongozi wa vyama vya siasa na wafuasi wao kuacha kuvuruga misiba ya wananchi, badala yake waitishe mikutano ya hadhara na kujinadi huko," alisema.

Baadhi ya misiba iliyokumbwa na malumbano hayo ni pamoja na mazishi ya Juma Mtumba aliyekuwa fundi umeme , mji wa Sirari na Fred Kimune.



# Watendaji waagizwa mikutano ya hadhara

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WATENDAJI wa vijiji na mitaa katika wilaya ya Singida wamekumbushwa kuitisha mikutano ya hadhara kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi bora ya mbegu ya alizeti ya ruzuku aina ya Record ili kuzitumia katika msimu huu wa kilimo.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Singida, Moses Machali, alitoa agizo hilo wakati akizungumza na madiwani, maofisa tarafa, maafisa ugani, watendaji wa kata na vijiji na mitaa wa halmashauri za Manispaa ya Singida na Wilaya ya Singida.

Alisema watendaji hao pia wawahamasishe wakulima katika halmashauri zao kujiandikisha katika daftari kupitia watendaji wa vijiji kwa ajili ya kupata mbegu hizo ambazo zitauzwa kwa fedha taslim na si mkopo kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Machali alisema mikutano hiyo itakayofanyika katika vijiji na mitaa, watendaji wafikishe ujumbe kwa wananchi jinsi gani serikali inavyowathamini wakulima kwa kuwaletea mbegu za ruzuku.

Pia aliwataka watendaji hao kupitia mikutano hiyo, kuwaorodhesha wakulima watakaotumia mbegu za ruzuku za Record na kiasi cha tani za mbegu kitakachotumika.

Machali alisema mkoa wa Singida umepatiwa zaidi ya tani 700 na kwamba endapo patatokea upungufu mawasiliano ya haraka yafanyike ili kupata nyongeza ya mbegu kutoka Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA).

Mkuu huyo wa wilaya aliagiza kupatiwa taarifa ya wakulima waliojiorodhesha kwa ajili ya kupata takwimu ya kiasi cha tani za mbegu zitakazoagizwa.

**Pia aliwataka watendaji hao kupitia mikutano hiyo, kuwaorodhesha wakulima watakaotumia mbegu za ruzuku za Record na kiasi cha tani za mbegu kitakachotumika**

# Tume ya ushirika yageukia kampeni upandaji wa miti

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imezindua mkakati wa upandaji miti kwa vyama vya ushirika ili kuunga mkono jitihada za serikali za kukabilina na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana baada ya kuzindua upandaji miti katika Shule ya Msingi Uhuru jijini hapa, Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alisema suala la mazingira ni ajenda ya kidunia ya kuhakikisha wanakabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Tumeona viongozi wetu wakituhamasisha kutunza, kulinda mazingira hasa upandaji miti hasa wakati wa mvua, sisi Tume ya ushirika tunaunga mkono jitihada za serikali katika kulinda mazingira na kuboresha mazingira," alisema.

Alisema tume hiyo inasimamia vyama vya ushirika nchini na vilivyopo hadi sasa ni 7,400 na suala hilo linatekelezwa nchi nzima.

"Tunahamasisha vyama vyenye mashamba viendelee kupanda miti na pia kwenda kupanda kwenye taasisi za umma. Shughuli za ushirika ni za kiuchumi na asilimia 60 ya vyama vya ushirika ni vya kilimo. Ili kuwa na kilimo chenye ustawi lazima kulinda mazingira na kwenye vyama vya ushirika vya mifugo ukiwa na ukame utakosa malisho na mifugo.

"Wanaushirika wanapaswa kulinda na kutunza mazingira ili kuimarisha uchumi, kama mlivyoona tuna uwakilishi hapa wa vyama vya ushiriki na tunakopa ili tukawekeze kwenye kilimo, mifugo na uvuvi kwenye mazingira mazuri,"alisema.

Ofisa kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Leonard Bilomo, alipongeza tume hiyo kwa juhudi hizo na kusisitiza kusimamia miti hiyo inayopandwa itunzwe na kukua.

Mmoja wa wanaushirika, Janeth Kalinga, aliahidi kutekeleza mkakati huo wa upandaji miti katika chama chake cha akiba na mikopo ili kulinda mazingira kwa vizazi vijavyo.



Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege akipanda mti katika shule ya msingi Uhuru, jijini Dodoma juzi, baada ya kuzindua mkakati wa upandaji miti kwa vyama vya ushirika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aonya wafanyabiashara rushwa

**Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida Peter Serukamba, amewataka maofisa biashara kujiepusha na rushwa katika utoaji wa huduma za leseni na usajili wa wafanyabiasha ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini.

Alisema hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya maofisa biashara kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Rukwa, Simiyu, Katavi na Tanga. Mafunzo hayo yana lengo la kuwajenga uwezo wa kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabishara hasa wakati wa utoaji wa leseni na kuwasajili.

Serukamba alisema maofisa biashara wafanye kazi kwa kufuata sheria ili kutoa huduma nzuri kwa wananchi kwa weledi na uaminifu mkubwa.

Alisema baadhi ya maofisa biashara wamekuwa wakitumika zaidi kama wakusanya mapato hasa sehemu za biashara, vilabu na kwenye nyumba za kulala wageni badala ya kuwa wasaidizi na washauri kwa wafanyabishara na wawekezaji.

Serukamba alisema serikali inatarajia kuona mafunzo hayo yanasaidia kubadilisha fikra na mitazamo ya maofisa biashara hao na watendaji wengine wa serikali ili waweze kutoa huduma kwa weledi na msaada kwa wafanyabishara badala ya kuonekana kama maadui kwao.

Mtendaji Mkuu Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa, alisema mafunzo hayo yana lengo la kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na maafisa biashara zinawafikia wananchi kwa karibu.

Nyaisa alisema endapo huduma hizo zitawafikia wananchi kwa karibu zitapunguza muda wa upatikanaji wa huduma hizo na gharama zisizokuwa za lazima katika urasmishaji wa biashara nchini.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo ambao ni maofisa biashara, walisema mafunzo hayo yatawasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabishara hasa wakati wa utoaji leseni na usajili wa biashara.

Walisema kupitia mafunzo hayo wataenda kutoa elimu kwa wafanyabishara ili kuendesha biashara zao kwa kufuata sheria za nchi na hivyo kuwavutia wawekezaji wengi kwenye maeneo yao ya kazi.





# Mpango ahimiza elimu bora maendeleo endelevu ya taifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, amesema elimu bora ndiyo inayowezesha uendelezaji wa rasilimali watu ili kuchangia kikamilifu katika kujenga taifa na kuleta maendeleo kwa ujumla.

Amesema ili kujenga jamii iliyoelimika na yenye maarifa muhimu, sekta ya elimu ni kipaumbele cha serikali zote mbili zinazoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk Hussein Ali Mwinyi, hivyo Wazanzibari wanayo haki ya kujivunia kwa hatua kubwa ya maendeleo iliyofikiwa katika sekta mbalimbali.

Dk. Mpango aliyasema hayo juzi wakati akizindua Shule ya Msingi ya Elimu Jumuishi ya Jendele, Mkoa wa Kusini Unguja, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema utekelezaji wa program ya elimu jumuishi ni hatua muhimu katika kutekeleza mpango wa maendeleo ya kitaifa Zanzibar na malengo endelevu ya dunia.

Alisema Zanzibar inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ikiwa imepiga hatua kubwa katika kutekeleza miradi ya sekta ya elimu kwa kuweka usawa katika upatikanaji wake kama ilivyo dhamira ya Mapinduzi.

Dk. Mpango alisema uwapo wa shule hizo ni muhimu kutokana na kujielekeza kutoa elimu kwa kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wasio na mahitaji maalumu.

Pia alisema tamko la haki za binadamu linatambua tofauti za kimsingi walizo nazo binadamu na linasisitiza kuwa zisifanywe kuwa vikwazo katika kufikia malengo.

"Kongamano la elimu ya dunia linahimiza na kusisitiza umuhimu wa shule kujumuisha watoto wote bila kujali hali zao za kimaumbile au kijamii," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, ujenzi huo ni jitihada za makusudi kukuza ushirikiano, uelewa na kuvunja mipaka iliyowekwa na jamii kuhusu ulemavu, hivyo kuacha tabia ya kuficha watoto wenye ulemavu majumbani, kuwapeleka shuleni kujifunza ili kuibua vipaji vyao na kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Dk Mpango aliahidi ofisi yake kulipia huduma ya umeme na maji kwa mwaka mzima wa 2024, katika shule hiyo ili kuimarisha huduma zinazotolewa hapo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, alisema serikali itaendelea kuweka mazingira bora, ikiwamo maslahi ya walimu na vifaa vya kisasa.

Pia alisema ujenzi huo umethamini na kujali wananchi wote kulingana na hali zao sambamba na kuhakikisha wananchi wote kupata elimu bila ya malipo kuanzia msingi hadi sekondari.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kasi ya ukuaji uchumi katika mkoa huo inakwenda sambamba na kasi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdallah Said, alisema ujenzi wa shule hiyo unakwenda sambamba na ujenzi wa shule nyingine kama hiyo Pujini kisiwani Pemba, uliojengwa kwa fedha za UVIKO -19.

Shule hiyo imejumuisha majengo saba yakiwamo utawala, madarasa, nyumba za walimu, kituo cha afya, sehemu ya chakula na dahalia ya wanawake na wanaume na imegharimu Sh. bilioni 3.7.

Wanafunzi 60 wenye mahitaji maalumu watasoma hapo na kwa sasa sasa Zanzibar ina wanafunzi wenye mahitaji maalumu 5,712, wa maandalizi na msingi.



Ofisa uthibiti wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Frank Kalili (kulia), akitoa maelezo kwa mwananchi aliyetembelea Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayofanyika katika Uwanja wa Dimani, nje ya mji wa Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mchechu asisitiza mabadiliko ya sheria kuimarisha Uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, amesema serikali itaendelea kubadili sheria ili kuendana na kasi ya uchumi anayoitaka Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Aliyasema hayo jana katika Ofisi ya Msajili wa Hazina, Maisara visiwani Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kujenga na kuimarisha ushirikiano baina yao.

Alisema serikali ipo katika mkakati wa kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi na ukuaji wa uchumi unaenda kwa kasi hivyo ni vyema kuwa makini katika kusimamia na kuweka mpango mkakati ili kufikia malengo.

Mchechu alisema ushirikiano kati ya Ofisi ya Msajili Tanzania na Zanzibar ni njia moja ya kuleta mabadiliko ya kukuza uchumi nchini.

Pia alisema lengo la ziara hiyo ni kubadilishana uzoefu na kupeana ujuzi wa kiutendaji katika kazi za kila siku ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano waliyotiliana saini Aprili, mwaka jana ili kuleta ufanisi.

"Ushirikiano kati yetu katika utendaji wa kazi zetu ni jambo lisiloepukika kwa vile sote tunafanya kazi moja ya kusimamia mali za umma," alisema Mchechu.

Msajili huyo alisema ni wajibu wao kuhakikisha taasisi zote za serikali zinafanya vizuri katika kusimamia mali za umma na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria endapo zitakwenda kinyume cha sheria za usimamizi wa mali za umma .

Katika kuimarisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, alisema wasajili wamekubaliana kuongeza weledi katika kusimamia mashirika kwa manufaa ya umma wa Watanzania.

Pia alisema wameamua kubadilishana wafanyakazi na uzoefu wa watendaji kitaalamu pamoja na kuwa kioo cha ufanisi wa utendaji kazi kwa kushiriki kikamilifu katika kudumisha Muungano.

Msajili wa Hazina Zanzibar, Waheed Muhammad Sanya, alisema ofisi yake kwa kwa sasa inasimamia mashirika 17 na imejipanga kuhakikisha mashirika hayo yanaleta tija kulingana na malengo ya kukuza uchumi.

## Majaliwa: Dhamira ni huduma bora za afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema dhamira ya serikali ya Zanzibar kuimarisha miundombinu ya sekta ya afya ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora katika mazingira bora na viwango vinavyokubalika.

Majaliwa aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa hospitali ya wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja katika eneo la Pangatupu ikiwa ni shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali itaendelea kuweka mifumo itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi lengo likiwa ni kuimarisha afya za watu.

Aidha alisema SMZ imeshajenga hospitali 10 za wilaya ili kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini na kupata huduma bora.

Majaliwa alieleza kuridhishwa na vifaa vilivyokuwapo katika hospitali hiyo na kusema kuwa vinakidhi vigezo vya hospitali ya wilaya.

"Nimeingia humu ndani nimeona vifaa kwenye idara zote, kiukweli vifaa vilivyomo humu ni vya hadhi ya juu sana kwa mfano idara za wagonjwa wa dharula kuna dharula za kila aina mpaka za watoto nimeridhishwa sana," alisema.

Pia aliwapongeza viongozi wa Wizara ya Afya kwa kutekeleza vizuri sera ya afya visiwani Zanzibar kwa kuisimamia miradi mbalimbali ya sekta hiyo inayotekelezwa.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kabla ya ujenzi wa hospitali hiyo eneo hilo lilikuwa la wazi na ilitolewa ahadi ya kujengwa hospitali na Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein.

Alisema hospitali hiyo itakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa, na kwa mara ya kwanza kuwa na hospitali yenye ICU ya kisasa ambayo ina uwezo wa kulaza wagonjwa sita kwa wakati mmoja na vyumba viwili vya upasuaji.

"Tunaamini sasa hakutakuwa na mgonjwa atakayepewa rufani kutoka katika wilaya hii kwa sababu ya ukosefu wa kitanda, huduma za upasuaji, huduma za wagonjwa wa uangalizi maalum (ICU). Huduma za dharura au vipimo vya msingi vinavyopaswa kufanyika katika ngazi ya hospitali hii itabakia historia na kupunguza gharama zinazotokana na rufaa zisizokuwa za lazima kwa wananchi na serikali yetu," alisema.

Alisema ufunguzi wa hospitali hiyo utasaidia katika utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wapatao 99,921 kutoka katika Shehia 31 za Wilaya ya Kaskazini B na maeneo jirani kwa lengo la kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma bora za fya kwa wote.



**CAREN SIMBA AMWACHIA MUNGU** Ukurasa 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JANUARI 13, 2024



# Wewe ungeweza?

PENGINE watu wanazidi kumuandama Harmonize ambaye anatuhumiwa kumpora mwanamke rafiki yake mkubwa DJ Seven.

Sakata hilo ambalo linazidi kushika kasi katika mitandao, limewagawa mashabiki wa muziki nchini ambao kuna baadhi wanamlaumu Harmonize na wengine wakimuona kuwa hana kosa lolote.

Katika sakata hilo, mwanamke anayetajwa kugombaniwa ni mrembo Posh Queen, ambaye umbo lake limekuwa mtihani kwa wanaume anaokutana nao.

Baadhi ya watu wamemtetea Harmonize, wakidai kwamba wa kulaumiwa ni Posh Queen, ambaye licha ya kujua kwamba wawili hao ni marafiki, ameamua kumsaliti mpenzi wake.

Jerry Philip kutoka Mbagala, amesema mwanamke ndiye alitakiwa kuwa na msimamo kwani anafahamu Harmonize na DJ Seven ni marafiki na hivyo hakupaswa kuwachanganya.

"Kama ni kweli  Harmonize hawezi kulaumiwa kwani mwanamke ndiye anajua mipaka na msimamo wake kuhusu mapenzi," amesema Philip.

DJ Seven ameacha kufanya kazi na Harmonize kutokana na kitendo cha mwanamuziki huyo kumchukua mwanamke wake Posh Queen.

BASI SAWA

## Simorix, afanya kolabo na...

RAPA mkali mwenye makazi yake nchini, Australia, Saimon Masanja, anayefahamika kama Simorix The General, amekamilisha kolabo na mastaa tofauti wakati akiwa hapa nchini.

Akizungumza na BT, Simorix amesema miongoni mwa wanamuziki nyota ambao amefanya nao kazi ni Jux, Gnako na wengine.

Hivi karibuni Simorix ameonekana akiwa karibu na wanamuziki Aslay na Mrisho Mpoto katika viwanja tofauti vya burudani.



## Terence asherehekea miaka saba bila bangi

MCHEKESHAJI na mwigizaji kutoka Kenya, Terence Creative, ameibua mjadala baada ya jana kusherehekea miaka saba tangu aache uvutaji wa bangi.



Kupitia kurasa zake wa Instagram, Terence aliandika ujumbe mzito akimshukuru bibi yake kwa kumpa mafunzo sahihi ambayo kwa sasa ameanza kuonekana bora mbele ya jamii.

"Leo nashukuru kwa safari kila hatua, changamoto, na ushindi umeunda vile nilivyo leo. Hapa ni kukumbatia njia iliyo kwa mikonoya wazi," amesema msanii huyo.





## Caren amuachia Mungu

MWIGIZAJI wa Bongo Muvi, Caren Simba, amesema kitu ambacho anakichukia katika maisha yake ni kufanya upasuaji wa aina yoyote katika mwili wake.

Akizungumza hivi karibuni Caren, amesema huwa anachukia pale watu wanapomnyooshea kidole wakidhani umbo lake limetokana na upasuaji.

"Hakuna kitu ninachokichukia ni kufanya upasuaji kwenye mwili wangu, lakini hilo watu hawaliamini wanabaki na mawazo yao pekee kwamba nimefanya hivyo. Siwezi kuzungumza sana ila kila kitu Mungu pekee anajua,@ amesema.

## Hiyari Yangu: Kibwaya ngoma si yako

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii iitwayo 'Hiyari Yangu', imechezwa na wasanii Simon Mwapagata, Suleiman Barafu, Wellu Sengo, Muhogo Mchungu na wengineo.

Mwapagata na mkewe Wellu wanaonekana kuishi maisha ambayo ni tofauti na ilivyozoeleka kwa jamii yetu ya Kiafrika baina ya mume na mke.

Mume anapika chakula, anafua nguo na kufanya kazi zote za ndani, huku mkewe akiwa ametulia tuli.

Hali hiyo inamkera mno kaka wa Mwapagata, aitwaye Barafu aliyekuja kuwatembelea, na anamkanya ndugu yake asiwe bwege. Hata hivyo yote hayo hayakusaidia, jamaa aliendelea na kazi zote za nyumbani, huku mke akiwa na kazi ya kupeleka watoto shule na kuwarudisha, lakini anaporejea anatulia tu nyumbani huku akichati na simu.

Hali ilipozidi kuwa mbaya, Barafu akaamua kuondoka nyumbani kwa mdogo wake kwani hakuweza kuvumilia hali ile. Akakimbilia kwa baba yake mdogo, Muhogo Mchungu na kumueleza kuwa mdogo wake amepewa limbwata na mkewe, kwani imefikia wakati sasa anakuna hadi nazi, mkewe akiwa amekaa tu.

Muhogo anaamua kufunga safari hadi kwa mtoto wa ndugu yake na kukuta yale yale aliyosimuliwa.

Pamoja na kumuweka chini mkewe akiwa hayupo, lakini Mwapagata hakusikia, aliendelea na kazi zake kama mtoto wa kike.


Alipoondoka wenyewe walicheka na kukumbusha na kuwa bado siku tatu tu.

Wellu, mke wa Mwapagata anaitisha kikao cha wanandugu wote, lakini wa kiume baadhi walisusa, kutokana na walichokiona. Kwenye kikao hicho Wellu alifafanua kuwa mumewe aliamua kufanya kazi zile kwa hiari yake kwa muda wa mwezi mmoja ambao yuko likizo ili kuangalia uzito na kazi za akinamama.

Akasema walikuwa wanabishana na mumewe kwa kuwa kuna wakati mke analalamika kuwa anachoka, hivyo akasema atakapopata likizo atakuwa akifanya kazi zote za ndani ili aone kama zinachokesha kweli au la.

Mwapagata alikiri hilo na kusema kuwa kesho ataanza kazi ofisini na kazi za ndani zitaendelea kwa mkewe kama kawaida na hali ile haikuwa kama wengi walivyotafsiri kuwa amelishwa limbwata. Wengi walishangaa na wambea wakabaki midomo wazi. Vizabizabina na visalata wa mtaa likawashuka.





## Ruby haambiwi kitu

MSANII wa Bongo Fleva, Ruby ameonyesha kwamba kile anachokisema kinatoka moyoni na uamuzi wake wa kutoolewa tena utabaki palepale.

Hivi karibuni Ruby aliongea na mashabiki zake kupitia Istagram na kusema hana mpango wa kurudi kwenye ndoa baada ya kuachana na Kusah.

Baadhi ya mashabiki walionekana kutofurahia na uamuzi wake huo na kumuomba kubadili mawazo kwa kuwa maisha ya ndoa yana changamoto zake.

Ruby amewajibu mashabiki hao kuwa hatakuwa mwanamke wa kuhisi hajakamilika bila ndoa, badala yake anaendelea kuimarika na kufanya mambo yake akiwa singo.

## Sumu ya Ali Kiba yazua balaa

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita kwenye safu hii kulikuwa na ngoma tano ambazo zilionekana kufanya vema mwaka jana.

Kichwa cha habari kilikuwa, 'Ngoma 5 zilizotikisa 2023.' Ngoma ambazo zilipigiwa upatu na kuwekwa hapa ni, 'Yatapita' wa Diamond Platnumz, 'Enjoy' wa Jux, akimshirikisha Diamond Platnumz, 'Pita Huku,' ulioimbwa na Dulla Makabila, 'Amepotea', uliopigwa na Mbosso na 'Tajiri', uliofyatuliwa na Lavalava.

Baada ya makala ile, baadhi ya mashabiki wakapiga simu na wengine meseji kuridhishwa na mtiririko ule, lakini wengi wakalalamika baadhi ya nyimbo hazipo, na zilipashwa ziwepo.

Wimbo ambao ulipata kura nyingi ambapo mashabiki wa muziki wa bongo fleva walikuwa wanautaka uwe mmoja wa nyimbo bora mwaka jana ni 'Sumu' wa Ali Kiba.

Kwa sababu wiki iliyopita kulikuwa na ngoma tano, leo naziweka tena zingine tano, ambazo zilikonya mioyo ya mashabiki wa muziki wa bongo fleva, nikianza na ule uliochaguliwa na kura nyingi zaidi.

**Sumu-Ali Kiba**

Ni wimbo aliomshirikisha msanii Mario na ukapandishwa Julai 14 mwaka jana.

Kiba anasema mke na mume wa mtu wote ni sumu, na kwenye jambo la mtu kaa mbali nalo.

Halafu anakwambia chunga sana katika dunia hii kuna hela na jela. Na wapo watu kwenye dunia hii anakula raha kwa kutumia pesa nyingi, lakini halipi madeni madogo madogo.

**Mambo matano-Lady Jaydee**

Huu ni moja kati ya wimbo uliopata kura nyingi baada ya ule wa Ali Kiba. Ulifyatuliwa Septemba 15 mwaka jana.

Mwanamama Lady Jaydee analia na mpenzi wake wa zamani. Anasema aliyataka mwenyewe kutengena na yeye, nanukuu baadhi ya mashari wa wimbo huo

"Nazi alitia kwenye chai, si alitaka mwenyewe kutengana na mimi? Hivi ni mnene au mwembamba, semeni nyinyi, hivi yuko sawa mnielezee? Mimi mjini sijaja kucheza, sifundishwi kupenda na wala sirudishi mateka." Sijui nani kaambiwa hiyo! Hatari, lakini salama.

**Falling-Nandy**

Nandy aliitoa ngoma yake hii Mei 19 mwaka jana. Ni wimbo wa mapenzi ambao nao uliwabamba mashabiki wengi wa muziki kiasi nao kupendekezwa kuwa moja kati ya pini zilizotikisa 2023.

**Utaniua-Zuchu**

Ukichachilia mbali wimbo huo, lakini video yake pia inaongeza ile hali ya kupendwa na mashabiki.

Video ya wimbo huo iliyotoka Mei Mosi, imekuwa kama filamu hivi. Mzee mmoja mnoko anayemsaka kijana Diamond aliyemtorosha binti yake Zuchu, ni moja kati ya vitu vilivyonogesha ngoma hiyo na kuwa kama si wimbo tu, bali filamu fulani hivi.

**Love Song-Marioo**

Mashabiki hawakuusahau 'Love Song' wa Marioo, aliomshirikisha Ali Kiba, akiupandisha kwenye mtandao wake wa instagram, Julai 31 mwaka jana. Japo kwa uchache, wakasema nao unafaa kuwa wimbo bora wa 2023.





# Keffe D aachiwa kwa dhamana

MAHAKAMA imemuachilia kwa dhamana Deane Davis maarufu kama Keffe D, mtu anayetuhumiwa kupanga na kutekeleza mauaji ya rapa maarufu nchini Marekami, Tupac Shakur.

Davis ambaye aliongoza genge la kihalifu katika eneo la Los Angeles, amepata dhamana ya kiasi cha dola za Marekani 750,000.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa Septemba 2023 kwa tuhuma za mauaji kwa kutumia silaha.

Kuachiliwa kwake kwa dhamana kunakwenda sambamba na ufuatiliaji mkali ikiwamo kuwekewa kifaa maalum cha kielektroniki na kuwa katika kizuizi cha nyumbani.



## Baba wa Mohbad adai kutishiwa maisha

BABA wa mwanamuziki wa Nigeria, Mohbad ambaye kifo chake kimejaa utata, amedai maisha yake yapo hatarini.

Joseph Ayoba amedai kwamba amekuwa akipata vitisho vya kukatisha uhai wake kutoka kwa mjane wa mwanawe Wunmi na wakili wake Femi Falana.

“Nahitaji haki kwa mwanangu na nataka watu waniunge mkono. Hili la kucheleweshwa kwa ripoti ya uchunguzi wa maiti na mambo mengine inaweza kusababisha kukanusha. Simwamini mtu kwa sasa. Hata kwa vitisho walivyokuwa wakinitumia Falana na mteja wake,” amedai Ayoba.

## Davido kwani una nini?

MPENZI wa zamani wa msanii wa muziki nchini Nigeria, Davido, amemfungulia mashtaka mwanamuziki huyo akidai kumfanyia vitendo vya unyanyasaji.

Wakili wa Sophia Momodu, ambaye ni mama wa mtoto mmoja, amemshutumu Davido kwa kumnyanyasa katika mtandao na kutishia usalama wa maisha yake.

“Tunaandika barua kuhusu mwenendo wa David Adeleke dhidi ya mteja wetu, ambao ni sawa na unyanyasaji wa mtandao, vitisho kwa maisha ya mteja wetu, Bi Sophia Momodu na washirika wake wa karibu,” imesema taarifa hiyo.





## Lupita hadi nyama ya nyoka!

MWIGIZAJI kutoka Hollywood mwenye asili ya Kenya, Lupita Nyong’o, ameibua mjadala baada ya kuonekana akisifia nyama ya nyoka.

Katika video iliyosambaa katika mitandao ya kijamii, inamuonyesha Lupita akiwa katika mtaa maarufu kwa uuzaji wa nyama ya nyoka nchini Benin, na alionekana akisifia ladha nzuri ya kitoweo hicho.

Katika video hiyo aliyoiweka kwenye ukurasa wake wa Instagram, aliambatanisha na ujumbe unaosema kwa mara ya kwanza na amekula nyama hiyo yenye protini hiyo isiyo ya kawaida, na yenye ladha tamu kama ya kuku.

## Will Smith amshangaza kijana kutoka Guinea

MSANII Nyota wa filamu kutoka Marekani, Will Smith, amemfanyia ‘sapraizi’ kijana mmoja kutoka Guinea, Mamadou Barry, kwa kumzawadia baiskeli na kompyuta.

Barry ambaye anasifika kwa kuzunguka bara la Afrika kwa kutumia baiskeli, alionekana kuwa kivutio kwa Smith na kuamua kumpatia zawadi hiyo na kisha kuzungumza naye kwa njia ya simu.

Smith alionyesha kuguswa juhudi zake na alipompigia simu Barry alionekana kuwa na furaha huku akishangazwa kumwona staa huyo akizungumza naye kwa upole.





## Wavuvi wapatiwa mkopo nafuu boti

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

SERIKALI imewapa faraja wavuvi wadogo wa wilaya ya Tanga, waliokuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu katika mwalo wa Deep Sea, baada ya kuwapelekea boti kubwa ya uvuvi wa kisasa yenye thamani ya Sh. milioni 121.

Akizungumzia ujio wa boti hiyo jana, Katibu Mtendaji wa Chama cha Ushirika cha Wavuvi na Wachuuzi katika mwalo huo, Bahero Adhio, alisema boti hiyo ni mahususi kwa ajili ya kuwawezesha kuendesha shughuli zao kwa tija zaidi.

Kwa mujibu wa Adhio, boti hiyo imenunuliwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na chama hicho kitalazimika kufanya marejesho pasipo na riba.

"Serikali imetoa zana nzuri za uvuvi na sisi wilaya ya Tanga tumepata 'Fibre Boat' kubwa HP 75, yenye urefu wa mita 14. Gharama yake ni Sh. milioni 116. Ukichanganya na bima na thamani ya Dola za Marekani, ndiyo unapata hiyo Sh. milioni 121," alisema Katibu huyo.

Adhio alisisitiza kuwa kupatikana kwa boti hiyo, kutawawezesha wavuvi kutoka kwenye uvuvi mdogo wa kuvua karibu, na sasa watakwenda kwenye kina kirefu.

Adhio ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi Wilaya ya Tanga (CHAWAWATA), alisema wameendelea kuwaelimisha wavuvi kujua mipaka yao kiutendaji sanjari na kuwaasa matumizi ya zana zisizohitajika katika uvuvi.

Alisema sera za CHAWAWATA ni kuunganisha wavuvi wadogo wadogo hususani vijana hatua ambayo inasaidia kutoa fursa kwao kupatiwa usaidizi.

# Wawindaji wasaidia waathirika Hanang'

**Na Jaliwason Jasson,**
HANANG'

JUMUIYA ya Kampuni za Uwindaji wa Kitalii Tanzania (TAHOA), imewapa mkono wa pole waathirika maporomoko ya tope, mawe na magogo yaliyoporomoka kutoka Mlima Hanang' mkoani Manyara, baada ya kuwapelekea mabati 1,143.

Mabati hayo ni mahususi kwa ajili ya kuiunga mkono serikali katika mpango wake wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa makazi mapya ya waathirika hao.

Kabla ya kukabidhi mabati hayo jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja, Katibu Mkuu wa TAHOA, Suleiman Masato, alisema jumuiya hiyo imeguswa na maafa hayo, hivyo kuamua kutoa msaada huo wa kibinadamu ili kuwawezesha wananchi waliokumbwa na maafa kurejea katika maisha ya kawaida.

"TAHOA licha ya kutoa msaada huu wa mabati, bado tunaahidi kuendelea kutoa michango mbalimbali ili kuwagusa waathiriwa hawa. Tumekabidhi mabati 1,143 yenye geji 28 za mita tatu, ambayo ni kiwango kinachokubaliwa na serikali," alisema Masato.

Huo ni mwendelezo wa TAHOA baada ya awali kutoa mchango wake Sh. milioni 47 ambazo ilikabidhi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama.

Maafa hayo yaliyotokea Desemba 3, mwaka jana, yalisababisha vifo vya watu 89 na kujeruhi vibaya wengine 139 katika mji wa Katesh, vijiji vya Jorodom, Ganana, Katesh, Dumbeta, Gendabi, Sarijandu, Arukushay na Sebasi.

Jumla ya kaya 207 zilizokuwa na wakazi 322, zimepoteza makazi katika maeneo hayo.

Baada ya makabidhiano hayo, Mayanja aliishukuru TAHOA kwa kuguswa na matatizo yaliyotokea wilayani hapa na kuunga mkono nia ya Rais Samia Suluhu Hassan, kujenga makazi mapya kwa wananchi hao.

"Mchango huu mliouleta umegusa maisha ya wananchi wa Hanang' waliopata maafa. Kama tunavyojua wengine wamepoteza makazi na vifaa mbalimbali. Nafahamu tayari mlishatanguliza mchango wa fedha katika akaunti ya maafa," alisema Mayanja.




Mtaalamu wa tiba za asili ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kliniki ya Kimataifa ya Tiba za asili ya Kazoba, Dk. Mwasiga Kazoba akifafanua jambo kuhusu namna dawa zake za asili zinavyofanya kazi kwa wagonjwa waliofika ofisini kwake, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Shule kitaifa ya wasichana kupokea wanafunzi Februari

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amesema ujenzi wa shule ya kitaifa ya wasichana inayojengwa Longido, mkoani Arusha kwa gharama ya Sh. bilioni tatu inatarajia kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Februari Mosi, mwaka huu.

Aidha, shule hiyo ambayo itakuwa mwarobaini wa ndoa za utotoni katika mkoa wa Arusha imepangwa kupewa jina la 'Longido Samia Girls'.

Mongella alisema hayo jana, alipokwenda kukagua shule hiyo yenye majengo zaidi ya 20 ya kisasa.

"Mkoa wa Arusha tulipokea Sh. bilioni tatu, kupitia Mradi wa Kuboresha Shule za Sekondari (SEQUIP) kwa lengo la kujenga shule ya kisasa ya wasichana ambayo ujenzi wake unaendelea kwa kasi na wanafunzi wanatarajiwa kuanza masomo Februari Mosi, mwaka huu," alisema.

Kwa mujibu wa Mongella, licha ya ujenzi wa shule hiyo kutokamilika kwa muda uliopangwa, wameongezewa muda hadi Februari 15, mwaka huu, na ofisi yake imejipanga kikamilifu kuongeza nguvu katika usimamizi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuhakikisha watoto wa kike wanapata elimu bora.

"Mapinduzi ya sekta ya elimu ambayo ni ndoto ya Rais Samia Suluhu Hassan, tumeyaona katika mkoa wetu wa Arusha, kwa kuwa shule nyingi mpya za msingi na sekondari zimejengwa pamoja na samani zake.

"Sisi wasaidizi wake tunaahidi kuunga mkono juhudi hizo kwa kusimamia kikamilifu miradi yote ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa ukiwemo huu wa shule ya wasichana inayojengwa hapa Longido ili watoto wa kike wapate elimu kwa kuwa ukielimisha mwanamke umeelimisha jamii nzima," alisema.

Kutokana na jiografia ya mkoa huo kuwa na idadi kubwa ya wafugaji, alisema watoto wa kike wako nyuma katika kupata elimu lakini kupitia shule hiyo, anaamini utakuwa mwarobaini wa watoto wa kike katika kupata elimu kwa kuwa itakuwa ya bweni.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Shule hiyo, Suppet Mseya, alisema vifaa vyote vya kukamilisha ujenzi wa majengo yote katika shule hiyo vimeshanunuliwa na kazi inayoendelea kwa sasa ni kusimamia mafundi kwa karibu, kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido ili watoto waweze kuanza masomo yao mara moja.

Salome Melubo, mmoja wa wananchi wanaoishi jirani na shule hiyo, alisema Rais Samia ni mwanamke jasiri ambaye ameonyesha dhamira ya dhati ya kukomboa mwanamke katika sekta mbalimbali.

"Tunamwombea sana mwanamke mwenzetu Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kutukomboa wanawake hasa sisi wa jamii ya kifugaji na kupitia shule hii ya bweni ya wasichana,.tunaamini watoto wetu wana uhakika wa kupata elimu na kuondokana na ndoa za utotoni.

"Katika jamii yetu ya kifugaji, mtoto wa kike anachumbiwa akiwa tumboni na wakati mwingine akiwa mdogo. Kwa hiyo akibahatika kumaliza elimu ya msingi, hata akifaulu anashinikizwa kwenda kwa mumewe na sisi wanawake tunakuwa hatuna sauti lakini sasa tumepata mkombozi,"alisema

TUNAVYOONA LEO USAFIRI DAR

# Sokoine, Mwaibula, Mwakyembe waliumiza vichwa vyao

**Na Adam Fungamwago**

WAKATI mwingine vitu vilivyotengenezwa au kupangiliwa vizuri tunavyoona leo siyo kama vilikuwa hivyo zamani.

Kuna watu walikuna vichwa, wakatumia usomi wao na kutatua tatizo kwa wananchi wanaowaongoza.

Ni kwa sababu Watanzania wengi hatuna tabia ya kuweka kumbukumbu na rekodi kwa baadhi ya watu waliofanya mambo makubwa kwa wananchi ili vizazi vinavyokuja vijue.

Rais wa Kwanza Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere alipata kusema kuwa usomi siyo kujaza vyeti na kuanza kutambia watu kuwa umesoma, ila uonekane kwenye jamii.

Alikuwa na maana kuwa mtu anaposoma anarudisha kwenye jamii kwa kwenda kuwasaidia wale ambao hawajapata bahati hiyo kuwatengenezea kitu, kuwapa elimu ya kile alichosoma au kuwapa utaratibu wa kufanya.

Msomi aliyetoka mjini au Ulaya na kurejea kijijini anaweza kuwaambia kuwa kumbe maji ya kisima inabidi yachemshwe na kuanza kusafisha vichaka ili kuepuka ugonjwa wa malaria.

Atawaambia kumbe watu wengi wanaokufa siyo kwamba wanarogwa, ni magonjwa ya kuhara kwa sababu ya kutochemsha maji na vichaka vya mbu.

Siyo anayerejea kijijini na kuanza kujishebedua, maringo, kujikweza, na kuchukua wake na mabinti wa watu.

Nchi hii ina wasomi wengi sana, lakini baadhi yao wanatumia usomi wao kwa kujiangalia wenyewe wao na familia zao, badala ya kuwasaidia wananchi na nchi kwa ujumla.

Nchini Tanzania miaka ya 1980, kulizuka shida ya usafiri kipindi hicho baada ya shirika pekee lililokuwa likifanya kazi ya kusafirisha watu jijini Dar es Salaam (UDA) kuzidiwa.

Kwanza kabisa abiria walianza kuwa wengi kutokana na kuongezeka kwa wakazi, lakini pia ubovu na uchakavu na mabasi huku pia kukiwa na ubadhirifu wa mali ya umma, ulisababisha kuwe na mabasi machache ambayo hayakukidhi matakwa ya usafiri.

Matokeo yake kukawa na foleni kubwa kila kituo cha jijini Dar es Salaam. Watu waliminyana kugombania mabasi kuliko hata tunavyoona kwenye baadhi ya matukio wa abiria wa Mbagala.



Mwakyembe



Sokoine



Mwaibula

Ikawa ni mshikemshike vituoni na kuwa mateso mkubwa kwa abiria hasa wanawake na watoto ambao hawawezi kugombania.


Miaka hiyo hiyo ya 1980, hadi mwanzoni mwa 1990 hakukuwa na usafiri wa kutoka Mwenge kwenda Gongo la mboto au kutoka Ubongo kwenda Kigamboni.

Badala yake abiria anayetaka kwenda kokote kule ilikuwa ni lazima atoke aliko kwenda Kariakoo kwanza au Posta na Stesheni ndiko unakoweza kupata usafiri wa kuunganisha kwenda sehemu nyingine.

Ukitoka Magomeni kama unataka kwenda Mbagala, kwanza ni lazima uende Kariakoo, Posta au Stesheni. Leo hii kuna ruti za kwenda sehemu yoyote ile moja kwa moja, bila kubadilisha mabasi.

Pia jijini Dar es Salaam hakukuwa na usafiri wa treni. Hivi sasa usafiri wa treni kutoka Stetesheni kwenda Ubungo na Pugu ndiyo ambao umekuwa mkombozi wa wananchi wengi.

Awali kulikuwa na msongamano mkubwa wa abiria katikati ya mji, hasa kariakoo na Posta, lakini kwa sasa wanaofannya kazi hata Msasani wanawahi mjini kwa ajili ya kupanda treni.



Vitu vyote hivi havijaja kwa bahati mbaya, kuna watu waliumiza vichwa na wakawa msaada sana kwa wananchi.

**Edward Moringe Sokoine**

Ni Waziri Kuu wa Tanzania kuanzia mwaka 1977 hadi 1980, na baadaye akarudi tena ofisini 1983 kabla ya kufariki kwa ajali ya gari Aprili 12, 1984.



Pamoja na mambo mengine yote, huku ndiye aliamuru watu binafsi waanze kubeba abiria jijini Dar es Salaam.

Baada ya kuona adha kubwa ya usafiri kama nilivyoeleza hapo mwanzo, akaona si vyema UDA kuendelea kufanya kazi iliyowashinda peke yao.

Akawataka watu binafsi wenye mabasi kuanza kusafirisha abiria. Na si wao tu, hata makampuni, mashirika, na taasisi binafsi na serikali ambayo yalikuwa na mabasi yakaruhusiwa kufanya biashara hiyo.

Sokoine anaendelea kukumbukwa kuwa ni mmoja wa viongozi ambaye amefanya kitu kinachoonekana kwa macho mpaka sasa, kuwa ndiye mwanzilishi mabasi ya daladala, baada ya kukerwa kuona wananchi wakiteseka na usafiri.

**David Mwaibula**

Alikuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Leseni za Usafirishaji Dar es Salaam. Ni mmoja wa watu ambao hawawezi kusahaulika hapa nchini hususan jijini Dar es salaam.

Huyu ndiye aliyeondoa adha ya abiria anayetaka kwenda eneo moja, hadi afike kwanza Kariakoo, Posta au Stesheni ili achukue usafiri mwingine.

Hivi sasa abiria ukitoka Makumbusho kwenda moja kwa moja hadi Kisemvule ujue mtu aliyesababisha hayo yote ni Mwaibula. Aliamua kutumia elimu na akili yake kusaidia wananchi na kuwafanyia maisha yao kuwa rahisi.

Ndiye pia alianzisha utaratibu wa kupaka daladala mistari yenye rangi ili kutofautisha eneo zinapotoa huduma, ambapo wakati mwingine hata asiyejua kusoma akiona mstari tu anajua hilo linakwenda wapi. Anabaki kwenye kumbukumbu muhimu nchini Tanzania.

**Dk. Harrison Mwakyembe**

Akiwa waziri anayehusika na mambo ya usafiri, akaangalia wananchi wanavyoteseka, akaona na yeye atumie uwezo, elimu na akili yake kwa ajili ya wananchi.

Badala ya treni kuwa za kwenda mikoani tu, akaamua pia ziwepo za hapa hapa Dar es Salaam kuwaokoa wananchi hasa nyakati za asubuhi, jioni na usiku.

Ndiyo maana kwa sasa kuna treni asubuhi na jioni kutoka mjini kwenda Ubungo na Pugu, ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa mkombozi na msaada mkubwa.

Ukiangalia ule umati unaokuwa kwenye treni nyakati hizo ndiyo utapata picha kamili.

Kwa sababu yeye ndiye aliyebuni, wananchi wala hawakuwa na choyo, wakaipachika jina treni inayosafirisha abiria jijini Dar, wakaiita 'treni ya Mwakyembe.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# Wanasheria waandamana kupinga ukaidi wa Rais Ruto

**NAIROBI,** KENYA

WANASHERIA wa nchini Kenya wameandamana kupinga kauli ya Rais William Ruto ambayo wamedai ina vitisho na kukaidi amri ya mahakama.

Mawakili hao waliandamana jana katika mji mkuu wa nchi hiyo wa Nairobi, wakitoka Mahakama ya Juu hadi ofisi ya kiongozi huyo.

Maandamano hayo yaliandaliwa na Chama cha Wanasheria nchini humo (LSK) na kuwahusisha mawakili wote wa mahakama.

Rais Ruto alikosolewa wiki iliyopita baada ya kutishia kutotii maagizo ya mahakama, akidai kuwa baadhi ya majaji ambao hakuwataja waliungana na wanasiasa wa upinzani kuzuia miradi inayoanzishwa na utawala wake.

"Rais wa nchi hayuko juu ya sheria. Kwa hivyo, hatutarajii azungumze kana kwamba kutii amri za mahakama ni upendeleo bali ni hitaji la kikatiba," alisema rais wa LSK Eric Theuri.

Theuri aliongeza kuwa LSK itafikiria kuanzisha mchakato wa kumuondoa madarakani Rais Ruto kwa kukiuka katiba ikiwa ataendelea na mashambulizi yake dhidi ya mahakama.

Tayari LSK imeunda timu ya wanasheria kwa ajili ya kuwasilisha ombi hilo kwenye Mahakama ya Juu dhidi ya Rais Ruto kwa kukiuka katiba.

Mawakili kadhaa maarufu nchini Kenya wamejiunga na maandamano hayo, akiwemo Makamu wa Rais wa zamani Kalonzo Musyoka na waziri wa zamani Eugene Wamalwa, ambao kwa sasa ni wanasiasa wa upinzani.

Jaji Mkuu Martha Koome na kinara wa upinzani Raila Odinga,walimuonya Rais Ruto wiki iliyopita kwa kitendo cha kukaidi amri ya mahakama na kwamba kutaanzisha machafuko nchini humo.

# Marekani, Uingereza waipiga Yemen wakitumia makombora, ndege vita

**WASHINGTON,** MAREKANI

VITA vinavyoendelea Ukanda wa Gaza kati ya vikosi vya Israel na wanamgambo wa Hamas, vinaashiria kuenea eneo la Mashariki ya Kati, baada ya jana ndege za kivita za Marekani na Uingereza kuishambulia Yeman.

Kundi la Wahouth ambalo linatawala Yemen, hivi karibuni walifanya mashambulizi dhidi ya meli za kibiashara zinazosafiri kupitia bahari ya Shamu kama kulipiza kisasi kwa Israel.

Taarifa kutoka makao makuu ya Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilisema vikosi vya jeshi la Marekani na Uingereza vilianza mashambulizi ya anga usiku wa juzi kuamkia jana dhidi ya waasi wa Houthi nchini Yemen.

Rais wa Marekani, Joe Biden amethibitisha kuwepo kwa mashambulizi hayo na kueleza kwamba yameanzishwa kwa maelekezo yake.

Alisema mapigano hayo yamelenga maeneo kadhaa nchini humo yanayotumiwa na waasi wa Houthi ambao wanahatarisha uhuru wa wasafari wa baharini katika moja ya njia muhimu za maji duniani.

Rais Biden, alisema mashambulizi hayo yalifanywa kwa pamoja na vikosi vya Marekani na Uingereza vikisaidiwa na nchi za Australia, Bahrain, Canada na Uholanzi.

Maofisa wa Marekani walionukuliwa na Shirika la Habari la Associated Press walizungumzia kufanyika kwa mashambulizi makubwa ya kulipiza kisasi kwa kutumia makombora ya kivita ya Tomahawk na ndege za kivita zilizopaa kutoka kwenye meli ya kivita.

Maeneo yaliyolengwa ni vituo vya vifaa, mifumo ya ulinzi wa anga na ghala za silaha.

Waandishi wa habari wa AP walioko mjini Sanaa walisikia milipuko minne, lakini hawakuona dalili zozote za ndege za kivita.

Wakazi wawili wanaoishi Hudaydah walisema walisikia milipuko mitano mikali.

Hilo ni shambulio la kwanza kutoka jeshi la Marekani dhidi ya Wahouthi nchini Yemen tangu kundi hilo linaloungwa mkono na Iran lianze kurusha ndege zisizo na rubani na makombora dhidi ya meli za mizigo katika Bahari ya Shamu mwezi Novemba.

Ofisa mmoja wa kundi la Houthi amethibitisha kupitia mtandao wa X, kwamba mashambulizi hayo yamefanywa sehemu yote ya Yemen.

"Uchokozi wa Marekani na Waingereza dhidi ya Yemen kwa kufanya mashambulizi kadhaa kwenye mji mkuu, Sanaa, mkoa wa Hudaydah, Saada na Dhamar," alisema Ofisa huyo wa Houthi, Abdul Qader al-Mortada.

Wakati huo huo, nchi ya Saudi Arabia imeitaka Marekani na washirika wake kujizuia ili kuepusha kuzidisha mzozo katika eneo la mashariki ya kati.

Vyombo vya habari vilinukuu taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje, ikieleza nchi hiyo inafuatilia kwa karibu hali hiyo katika hali ya wasiwasi.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, imelaani mashambulizi yaliyofanywa dhidi ya Yemen na kusema ni ukiukaji wa wazi wa mamlaka ya Yemen na sheria za kimataifa.

"Mashambulizi hayo hayatakuwa na matokeo yoyote zaidi ya kuchochea ukosefu wa usalama na utulivu katika eneo hilo," alisema msemaji wa wizara hiyo, Nasser Kanani.

Wakati huo huo kundi la Hezbollah la Lebanon linaloungwa mkono na Iran pia limelaani mashambulizi dhidi ya Yemen.

"Uchokozi wa Marekani unathibitisha kwa mara nyingine tena kwamba Marekani ni mshirika kamili katika majanga na mauaji yaliyofanywa Israel huko Ukanda wa Gaza ", lilisema taarifa ya kundi hilo.

**BBC**



Waziri wa Sheria wa Afrika Kusini, Ronald Lamola na balozi wa nchi hiyo Uholanzi, Vusimuzi Madonsela wakiteta jambo ndani ya Mahakama ya Haki ya Kimataifa wakati wakifuatilia kesi waliyoifungua dhidi ya Israel jana. **PICHA: GETTY IMAGE**

# Burundi yafunga mpaka wake na Rwanda

**BUJUMBURA,** BURUNDI

Burundi imetangaza kufunga mpaka wake na Rwanda, baada ya wiki mbili zilizopita kuituhumu nchini hiyo kuunga mkono waasi waliofanya mashambulizi kwenye ardhi yake.

Hata hivyo, Rwanda imepinga madai hayo na kueleza hatua hiyo hiyo inakiuka kanuni za ushirikiano.

Serikali ya Burundi ilisema kundi la waasi la Red Tabara lilifanya shambulizi Desemba 22 mwaka jana karibu na mpaka na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kuua watu 20.

Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye ameishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi hao, madai ambayo serikali ya Rwanda imeyakanusha mara kwa mara.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Matin Nitereste, aliwaambia waandishi habari juzi jioni kwamba wameamua kufunga mpaka na Rwanda na kuonya yeyote anayejaribu kupitia mpaka huo hatofanikiwa.

Waziri Nitereste aliongeza kuwa baada ya kubaini nia yao mbaya, Rais wa Rwanda, Paul Kagame, walisitisha uhusiano wote hadi atakaporejea kwenye mstari.

Alisema Rwanda inawahifadhi wahalifu wanaowadhuru watu wa Burundi, na kuongeza kwamba wao pia hawawataki raia wa Rwanda.

**DW**

HABARI TANGAZO

# Zanzibar ilivyopiga maendeleo ya Afya

**Na Mwandishi Wetu**

AFYA ni msingi mkuu wa maendeleo endelevu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ni dhahiri kwamba bila jamii kuwa na afya bora hakuna maendeleo ya aina yoyote.

Zanzibar leo ikiwa inatimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya mwaka 1964, moja ya mambo ya kujivunia katika kipindi hicho ni maendeleo katika sekta ya afya. Yako mambo mengi ya kujivunia katika sekta hiyo na hata kuigwa na watu wengine kutokana na kile Zanzibar ilichokifanya katika afya ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi.

Akizungumzia maendeleo na mafanikio ya sekta ya afya katika miaka 60 ya Mapinduzi hivi karibuni, Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, anasema dhamira ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanakuwa na uhakika wa afya bora ikiwamo kupata matibabu bure, ina historia ndefu tangu wakati wa harakati za kupigania uhuru wa visiwa hivyo.

"Historia hii inaanzia wakati wa harakati za kujikomboa kutoka utawala wa kikoloni. Chama cha Afro Shiraz (ASP) katika manifesto (ilani) yake ilikuwa ikijinadi kwamba ikishinda afya na elimu vitakuwa bure kwa wananchi wa Zanzibar.

"Watu wengi walikuwa wa kipato cha chini, hivyo wasingeweza kupata matibabu sahihi. Baada ya Mapinduzi, Sheikh Abeid Amani Karume (Rais wa Kwanza wa Zanzibar) alitangaza kuwa matibabu ni bure. Alipiga marufuku hospitali binafsi na zikafungwa, wamiliki wakaondoka," anasema.

Kutokana na hali hiyo, kwa mujibu wa Mazrui, tangu wakati huo tegemeo kubwa katika matibabu lilikuwa serikali ambayo ilitoa dawa, vifaa tiba, matibabu bure, madaktari na wauguzi.

"Tukirudi nyuma kidogo, kabla ya Mapinduzi, Karume alikuwa Waziri wa Afya na baada ya Mapinduzi, Aboud Jumbe (Rais wa pili wa Zanzibar) alikuwa Waziri wa Afya. Sera ya Afya ilianzishwa na ikapelekwa Baraza la Mapinduzi na kila baada ya miaka 10 ilikuwa ikifanyiwa marejeo hadi sasa mimi nikiwa Waziri," anabainisha.

**KABLA YA MAPINDUZI**

Waziri Mazrui anasema huduma za afya Zanzibar zilianza mwaka 1884 baada ya ujio wa wakoloni ilipojengwa hospitali ya misheni kwa ajili ya kutibu wazee na watoto waliokuwa katika hali mbaya karibu na kufa.

Baada ya hapo, anasema mwaka 1890, mfanyabiashara Sewa Haji alijenga hospitali katika jengo kongwe kwenye Hospitali ya Kuu ya Mnazi Mmoja kabla ya Muhimbili, Dar es Saaam kwa gharama ya Rupee za India 3,000 kwa wakati huo.

Kwa mujibu wa Mazrui, kabla ya Mapinduzi, hali ya huduma za afya ilikuwa duni na vifo vilikuwa vingi hasa kwa watoto. Anatoa mfano wa mwaka 1919 walipofariki watoto 400 hadi 500 kati ya 1,000 hali ambayo ilisababisha kuanzishwa kwa Chama cha Wakunga Zanzibar (ZMA). Chama hicho kilikuwa na lengo la kupunguza vifo vya uzazi hasa maeneo ya vijijini ambako vilikuwa vingi.

Pia anasema kulikuwa na ushajihishaji wa ujenzi wa vituo vya afya ili kuwezesha wananchi kupata matibabu. Mwaka 1907 wakati wa utawala wa Sultan, anasema vilijengwa vituo vya afya vya serikali vilijengwa Makundichi na Mkokotoni vyenye uwezo wa kulaza wagonjwa 10 hadi 15 kwa wakati mmoja.



*Waziri wa Afya Zanzibar Mhe. Nassoro Ahmed Mazrui*

Uingereza ilipochukua madaraka, anasema ilijenga hospitali nne ambazo kwa kiasi kikubwa zilisaidia kwa kiasi fulani kupunguza changamoto za ukosefu wa huduma za afya. Hata hivyo, anasema kulikuwa na uhaba wa wafanyakazi, hivyo yaliandaliwa mafunzo ya haraka kwa wahudumu wa afya.

Maendeleo zaidi katika sekta hiyo yalionekana kati ya mwaka 1920 na 1930 baada ya kujengwa vituo 30 vya afya Unguja na Pemba pamoja na kuwapo magari ya wagonjwa.

"Lakini jambo ambalo lina historia kubwa kwa Zanzibar ni kwamba ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki kuwa na matibabu ya afya ya akili. Inasemekana mtoto wa Mfalme wa Uingereza alipata tatizo la akili na huduma hiyo ikaanzishwa. Pia kulikuwa na kliniki za meno Zanzibar wakati wa ukoloni," anabainisha Mazrui.

Pia anasema mwaka 1930 hospitali binafsi mbili na vituo vya kutolea huduma za afya vilianzishwa na baada ya hapo viliongezeka zaidi kwa sababu ilionekana soko lilikuwapo kwa watu wenye uwezo kifedha.

Aidha, mwaka 1958 hospitali ya Karimjee ilijengwa Cheke Chake na baadaye zilijengwa hospitali zaidi Chake Chake na Wete muda mfupi kabla ya Mapinbduzi.

**MAENDELEO YA SASA**

Mazrui anasema wakati Zanzibar inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu, kuna hatua kubwa katika maendeleo ya sekta ya afya. Anabainisha kwamba kwa sasa kuna vituo vya kutolea huduma 163 zikiwamo zahanati 129 na vituo vya afya 34.

Katika vituo hivyo, anasema kuna huduma mbalimbali kama vile afya ya mama na mtoto (MCH) ikiwamo kujifungua katika zahanati, vipimo na uchunguzi wa magonjwa. Katika vituo vya afya kuna majengo ya wagonjwa wa nje (OPD), maabara zenye vifaa vya kisasa, na huduma za uzazi.

"Kwenye vituo vya afya kuna huduma za uzazi kama huduma za wajawazito, kujifungua na baada ya kujifungua. Vituo vya huduma za afya vinapatikana chini ya kilometa tano na vimeenea sehemu nyingi tofauti na ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi," anasisitiza.

**FEDHA ZA UVIKO**

Kutokana na athari za UVIKO- 19 katika sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, Mazrui anasema serikali kupitia ilielekeza nguvu katika ujenzi wa hospitali ngazi ya wilaya katika wilaya 10 za Unguja na Pemba.

Hospitali hizo, anasema kila moja ina uwezo wa kulaza wagonjwa 100 hadi 120 kwa wakati mmoja na zina maabara za kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali, vyumba viwili vya upasuaji, kimoja kwa ajili ya kinamama ili kupunguza vifo vya uzazi.

"Pia kuna ICU (vyumba vya wagonjwa wa uangalizi maalumu) kwa watoto njiti na wenye uzito mdogo. Pia kuna huduma za mionzi, ultra sound, vipimo vya moyo (ECHO) vyote hivi vya kidijitali. Kuna vyumba vya kuhifadhia maiti na huduma za uchunguzi wa maiti (postmortem).

"Awali kulikuwa na ICU moja yenye vitanda vinane lakini sasa kuna ICU 14 zenye vitanda 80. Mwaka 2021 kulikuwa na vitanda 1,445 sasa kuna vitanda 2,645. Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja pekee ina vitanda 750 na kuna huduma ya mama na mtoto, na matibabu ya macho. Hii ni hatua kubwa sana iliyofikiwa na ya kujivunia ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi," anasema.

Licha ya mafanikio hayo, Waziri Mazrui anabainisha kwamba vyumba vya upasuaji vimeongezeka kutoka 11 hadi 35 vikiwamo 13 maalum kwa ajili ya kinamama. Pia kulikuwa na eneo moja la huduma za dharura lakini sasa yako 11.

**MIPANGO YA BAADAYE**

Katika kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuleta matokeo chanya kwa maendeleo, Mazrui anasema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imejipanga kufanya mambo makubwa zaidi. Moja ya mipango hiyo, anasema ni kupunguza mrundikano wa wagonjwa Mnazi Mmoja kwa kuziwezesha hospitali za mikoa kuwa za rufani.

Msisitizo mkubwa katika mpango huo, anasema ni kuimarisha afya ya msingi kwa kuhakikisha zahanati zina viwango, vifaa tiba na dawa za kutosha pamoja na rasilimali watu.

"Mpango wa sasa wa mwaka 2023 hadi 2025 ni kuhakikisha kila Jimbo lina kituo cha afya, hivyo mkakati ni kuwa na vituo vya afya 50 ifikapo muda huo. Pia kuwa na hospitali za mikoa katika kila mkoa. Chake Chake na Wetu ujenzi wa hospitali hizi utaanza wakati wowote.

"Hospitali ya Mnazi Mmoja itakuwa hospitali ya kisasa na nusu ya majengo yatavunjwa na kujengwa mpya ili kuifanya kuwa ya rufani kwa Unguja na Pemba. Hospitali ya Bumbwini pia itakuwa ya rufani," anasema.

Waziri pia anabainisha kwamba kumekuwa na ongezeko la watoto wanaozaliwa wakiwa na tatizo la moyo. Kutokana na tatizo hilo, anasema serikali imeamua kujenga hospitali kwa ajili ya matibabu ya maradhi hayo na kwamba eneo limeshatengwa na michoro imeshakamilika kwa ajili ya ujenzi.

Mpango mwingine, anasema ni kuongeza rasilimali watu kwa maana ya madaktari bingwa wabobezi, madaktari bingwa, mdaktari na madaktari wasaidizi, wauguzi, wafamasia na wataalamu wa mionzi na baabara.

"Kufikia mwaka 2027, lengo ni Zanzibar kuwa na rasilimali watu ya kutosha katika afya. Tunataka kupiga hatua kubwa zaidi katika hili. Kabla ya Mapinduzi madaktari na wauguzi walikuwa wazungu na wale wa asili ya kiasia. Waafrika walikuwa wachache, mwaka 1935 alikuwapo mwafrika mmoja tu, Kingwabi Hassan," anasema.

Kwa ujumla, hatua iliyofikiwa katika sekta ya afya tangu Mapinduzi mwaka 1964 ni makubwa na ya mfano wa kuigwa. Pia kwa mipango iliyopo, ni dhahiri kwamba miaka michache ijayo, kutakuwa na hatua kubwa katika maendeleo ya afya ambayo yatasababisha kuwapo kwa maendeleo kwenye uchumi na kijamii visiwani humo.


SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA

MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA MAPINDUZI
1964 - 2024



Mh. Dr.Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

WAZIRI, BODI, MENEJIMENT NA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA AFYA ZANZIBAR, WANAMPONGEZA DKT HUSSEIN ALI MWINYI RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI PAMOJA NA WANANCHI WOTE WA ZANZIBAR KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 60 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA MWAKA 1964

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-**10**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwangoo**

Akili yake kwa haraka haraka ilimtuma kuwa walikuwa wanamteta. Hakukosea. Alinyata taratibu akiambaambaa na ukuta wa nyumba.

Kabla ya kukata kona ambapo ndipo walipokuwa wamekaa upenuni mwa nyumba yake, sikio lake liliwasikia vizuri.

Maneno waliyokuwa wanaongea juu yake walimfanya kufura kwa hasira.

Alivumilia ili aendelee kuwasikia, lakini baadaye subira ikatoweka. Akajitokeza ghafla.

"Yaani nyingi wanawake wazima badala ya kufagia vyumba vyenu vilivyojaa vilivyojaa chawa, kunguni, viroboto na mende kazi mmekalia ubea hapa, halafu mnajifanya mnasukana."

Kujitokeza kwake ghafla na kusema aliyoyasema waliwafanya Tabia na Rozi kupatwa na mshtuko.

Hawakutarajiwa kitu kama kile kwa muda ule. Hawakutegemea kama mama mwenye nyumba yao atakuwa anawasikia wanayoongea.

Walimuona alivyoondoka, lakini hawakutegemea kama anaweza kurejea na kuanza kuwanyatia na kusikiliza wanavyoongea. Kikubwa ambacho walitambua ni kwamba amesikia maongezi yao yote. Akili yao sasa ikawatuma ama kuwa wapole au kujibu kila shambulio linalokuja kwa ajili ya kujilinda.

"Hivi mlijua siwezi kusikia?" Mwantumu akauliza.

Mpaka wakati huo hakuna yoyote aliyeongea wala kujibu kitu.

" Unatuuliza sisi, wewe kwako umefagia, maana tangu asubuhi ndiyo kwanza unarudi!" Rozi alijitutumua akajibu.

"Nenda kaangalia ndani mwangu, kunanukia maua ya yasmini dada, nimefagia nimetandika kitanda, nimepulizia manukato na maua nimemwagia kitanani, kwenu uvundo tu, mnakaa hapa eti mnasukana kumbe mmekalia umbea."

Lilizuka varangati la aina yake, watu wakatiana mkononi. Kwa sababu Rozi na Tabu walikuwa wawili, walimzidi nguvu mama mwenye nyumba wao.

Hadi wanaume walipokuja kuamua Mwantumu alikuwa amepigika. Mbio akakimbia polisi. Rozi na Tabu wakatiwa mbaroni. Walikuja kuachiwa kesho yake kwa dhamana.




Badala ya kuongea na kuchambana, sasa mfumo wa nyumba hiyo ulibadika, Walinuniana. Mwenye nyumba na wapangaji wakawa hawaongei. Kila mtu kivyake. Wanapishana kama magari yaliyojaa.

Waliokuwa wanazungumza ni wenyewe tu wapangaji. Mama kwenye nyumba waliwanunia wapangaji wake wote.

**********************************

"Nasema hivi nina uhakika kuwa mume wangu kafungiwa humu ndani."

"Kwa nini unasema una uhakika mama?"

"Ndiyo?"

"Sasa shida yako ni nini na umejuaje?"

"Mimi shida yangu mlango ufunguliwe nihakikishe yumo au hayumo. Na ushahidi kama yumo humu, hii hapa ni bodaboda yake, ameinunua wiki hii hii, imepaki hapa nje, sasa kaenda wapi? Na mimi usinione mjinga nimekuwa nikifuatilia meseji zake na huyo mpumbavu mwenzake, we unafikiri nijuaje kama amekuja hapa?" Ilikuwa ni sauti ya Devota ambaye alikuwa anaulizwa na mzee mmoja wa makamo.

Devota, akiwa amewakusanya akimama na kinadada mtaani kwao na wale waliokutwa njiani na wamba kibao walifika hapo kwa lengo la kufumania.

Kumfumania mumewe na Mwadawa, binti ya mama mwenye nyumba wake.

Haikuwa rahisi kwanza Devota kuamini hili. Awali alijua mumewe huenda ana mipango au mahusiano na mama mwenye nyumba.

Baadaye ndipo alipogundua kuwa mama alikuwa ni kuwadi wa binti yake.

Na hii ni kwa sababu ya kuzifuma meseji za mapenzi za binti huyo na mumewe. Hakuamini, alidhani labda mama mwenye nyumba wake anatumia namba ya binti yake.

Wale waliompa taarifa kuwa walimuona mumewe na mama mwenye nyumba wake kule Magomeni Uwanja wa Barafu walikuwa sahihi, lakini kuonekana kwao kuliwafanya watu wahisi wao ndiyo wapenzi. na ndiyo maana Devota mara kwa mara alikuwa anagombana na mumewe pamoja na kumchana mama mwenye nyumba wake kuhusu hilo.

Meseji alizoziona na kuanza kuzifanyia kazi zilimthibitishia kuwa mumewe alikuwa na mpango wa Mwadawa na wala siyo mama mwenye nyumba wake.

Safari hii hakupiga kelele baada ya kuiona meseji ikionyesha watakapokutana.

"Mke wangu wiki ijayo anakwenda kwenye harusi ya mtoto wa shangazi yake, utakuja basi kulala kwangu." Hiyo ilikuwa ya mumewe.

"Akaa mwenzangu, weee, yaani nije kulala chumbani kwako, chumba cha mkeo, akija ghafla itakuwaje, hapana, hiyo sitaki."

> **Niko peke yangu, mimi nimeachiwa chumba na shoga yangu Zai, yeye amekwenda msibani, sasa huyu mama na wenzake na umati wote huu umetoka huko umevamia hapa unasema mimi nimechukua mume wa mtu!**

"Basi chumbani kwako!"

"Sitaki pia, nimekwambia hivi, hapa hapa nyumbani hapana, iwe mbali na hapa, hivi nikwambie hivi mtu akituona itakuwaje? Na hapa unaona tayari pameshachafuka watu hawaelewani!"

Hii ilimpa picha kuwa zoezi hili lilikuwa linataka kufanyika kwa mara ya kwanza.

Tayari Mwantumu alikuwa ameshaifanya kazi yake vizuri ya kuwaunganisha binti yake na mume wa mpangaji wake Devota. Alichokuwa hakijui ni kwamba mume wa Devota alikuwa mzembe kiasi kwamba meseji zake zilikuwa zikinaswa kirahisi na mkewe, hivyo kila kitu kilikuwa mkononi.

Devota alichoamua ni kutengeneza fumanizi na si kubwata na kuzima zoezi kabla halijafanyika.

Akawaambia mashoga zake watiifu ambao ni wapangaji wenzake, wote wakakubaliana naye.

Siku ya tukio mume wa Devota akiwa na bodaboda yake akamuaga mkewe kuwa anakwenda kazini na kwa sababu kazi zitakuwa nyingi atakaa huko kwa siku tatu.

Lakini kumbe mkewe alikuwa anamg'ong'a, alijua anakwenda kwenye nyumba ambao ipo mtaa wa nne kutoka pale walipo.

Na hiyo ni baada ya kuifuma meseji moja iliyoharibu kila kitu.

"Shoga yangu Zaina amefiwa na mama yake mdogo, anakwenda Buza kuzina atakaa siku tatu, ameniachia chumba chake kwa hiyo kesho saa 12:00 jioni uje, muage mkeo sijui utaagaje, lakini nataka tufurahi kwa siku tatu, hakuna kutoka ndani. Chakula tunaagiza tu."

Kundi zima lilifika kwenye nyumba hiyo inayosemekana kuwa msichana yupo ndani na mume wa mtu.

"Kwani wewe msichana upo na nani humo?" Yule mzee ambaye alikuwa anakaa nyumba jirani akauliza.

"Niko peke yangu, mimi nimeachiwa chumba na shoga yangu Zai, yeye amekwenda msibani, sasa huyu mama na wenzake na umati wote huu umetoka hupo umevamia hapa unasema mimi nimechukua mume wa mtu!" Mwadawa alijibu akiwa dirishani.

"Sasa mbona umejifungia kama hakuna mtu humo ndani?" Akauliza tena mzee huyo.

"Nimejifungia kwa sababu ya usalama wangu wala siko na mwanaume humu ndani. Yaani kundi lote hilo wanataka kunivamia mimi wanipige!"

"Unawafahamu hawa waliokuja?"

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KAPAMA, ILANFYA WATUA KUIOKOA MTIBWA SUGAR

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inarejesha makali na kujinusuru na janga la kushuka daraja, Mtibwa Sugar imemalizana wachezaji wanne katika dirisha dogo la usajili akiwamo, Nassor Kapama kutoka kwa Wekundu wa Msimbazi, imefahamika.

**Nyota wengine wanaotaka wametua katika kikosi hicho cha Manungu mkoani Morogoro ni pamoja na kipa, Justine Ndikumana, aliyeachana na Coastal Unioni, Rashid Juma na Charles Ilanfya kutoka Ihefu.**

Usajili huo umefanyika kwa kuzingatia ripoti ya Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, ili kuboresha kikosi chake ambacho kilionekana kina mapungufu katika eneo la kipa, beki, kiungo na mshambuliaji.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Abdulrahman Said, aliliambia Nipashe usajili huo umefanyiwa kazi kutokana na ripoti waliyoipokea kutoka katika benchi la ufundi linaloongozwa na Katwila.

Said alisema wanahitaji kuboresha kikosi cha timu hiyo baada ya kuona mapungufu ya kikosi walipocheza mechi za mzunguko wa kwanza ambapo walipata matokeo mabaya na kufanya kuburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mashabiki wa Mtibwa Sugar wawe na subira, tunafanya maboresho ya kikosi chetu na kila kitu kitakuwa sawa, tutaweka wazi, hatuko katika nafasi nzuri kwenye msimamo, tumepokea ripoti na tayari imefanyiwa kazi ili kuboresha timu yetu ili kuhakikisha duru la pili tunafanya vizuri na kuendelea kusalia kwenye ligi," alisema Said.

Katwila alithibisha kuhitaji wachezaji katika nafasi hizo na anaimani viongozi wanaendelea na usajili kwa ajili ya kuimarisha timu yao.

"Siwezi kusema juu ya nyota hao uliowataja kwa sababu ripoti yangu nimeeleza nafasi tu ninazohitaji, yoyote nitakayeletewa niko tayari kufanya naye kazi, kikubwa ni kuhakikisha tunaitoa timu kwenye nafasi iliyopo chini ya msimamo na kujiweka mahali pazuri ili tubakie katika msimu ujao wa ligi," alisema Katwila.

Azam FC yenye pointi 31 ndio inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga wenye pointi 30 na Simba yenye pointi 23 ikiwa katika nafasi ya tatu.

Hata hivyo, Azam imecheza mechi 13 wakati Yanga imeshuka dimbani mara 11 huku Simba ikicheza michezo 10 tu.

# KMC kuanika nyota wapya

**Na Saada Akida**

WAKATI aliyekuwa winga wa Simba, Peter Banda akihusishwa kutua KMC FC, uongozi wa timu hiyo umesema leo utaweka wazi hatua waliyofikia katika mchakato wa usajili wa nyota wapya kutokana na ripoti waliyopokea kutoka kwa Kocha Mkuu, Abdihamid Moalini, imeelezwa.

Banda pia alikuwa akihusishwa kutakiwa na Singida Fountain Gate FC, lakini timu hiyo bado inatumikia adhabu ya kufungiwa kusajili iliyopewa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa KMC, Daniel Mwakasungula, alisema klabu hiyo itaweka wazi wachezaji na mipango yao ya usajili leo ili kuanza maandalizi ya ligi na hatimaye kufikia malengo.

Alisema wamefanyia kazi mapendekezo ya usajili yaliyotolewa na kocha wao ambaye pia aliweka wazi baadhi ya wachezaji wanaotakiwa kutolewa kwa mkopo ili kwenda kupata uzoefu na baadaye kurejea kuisaidia timu.

"Kwa sasa hatuwezi kuweka wazi nani tumemsajili na yupi anatolewa kwa mkopo, lakini tumefanya usajili kulingana na kile kilichotufikia kutoka katika ripoti ya kocha wetu (Moalini), kesho (leo) tutaweka wazi nani atakuwa sehemu ya kikosi kikosi chetu cha KMC," alisema Mwakasungula.

Aliongeza wanaamini usajili huo utakifanya kikosi chao kiwe tayari kukabiliana na ushindani uliopo huku pia kikidhamiria kumaliza katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi.



Kipa wa Simba Queens, Zubeda Mgunda (kushoto), akifurahia jambo katika mazoezi ya timu yake kuelekea mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Amani Queens itakayochezwa Januari 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi. **PICHA: SIMBA SC**

## Hatimaye Lusajo aibukia Mashujaa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya tetesi za muda mrefu, straika, Relians Lusajo, ametambulishwa rasmi kujiunga na Mashujaa FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Lusajo amejiunga na Mashujaa baada ya kuachana na timu yake ya zamani, Namungo FC.

Ofisa Habari wa Mashujaa, Hamisi Milyango, alisema wamemsajili Lusajo kutokana na mahitaji ya timu na kuridhishwa na kiwango chake ambapo wanaamini atasaidiana vyema na Adam Adam.

"Tumemwongeza straika wa mabao, Lusajo ambaye naamini atakuja kutuongezea nguvu kwenye kikosi chetu, mwalimu, Mohamed Abdallah 'Bares' alihitaji mtu kama huyo ili kumsaidia Adam Adam," alisema Milyango.

Baada ya kutangazwa, Lusajo aliyehusishwa kujiunga na Simba, Azam na Singida Fountain Gate, aliwashukuru Namungo kwa muda wote aliokuwa nao na kuongeza alihitaji kubadilisha upepo.

## Bodi yataka viwanja Ligi Kuu virekebishwe

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema itavifungia viwanja vyote ambavyo havitarekebishwa kipindi hiki ambacho ligi imesimama.

Taarifa iliyotolewa na TPLB jana imesema inazitaka timu kutumia fursa ya mapumziko ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kufanya marekebisho kwenye viwanja vinavyochezwa mechi za Ligi Kuu ili kuendelea kutumika.

Bodi hiyo imezitaka klabu zote kuhakikisha zinafanya maboresho kwenye viwanja vyao hasa maeneo muhimu ya kuchezea (pitch), uzio wa kutenganisha eneo la kuchezea na mashabiki, vyumba vya kuvalia, majukwaa ya mashabiki na ya watu maalum, vyoo vya halaiki, na vya watu maalum, muilango ya kuingilia na kutoka uwanjani na maeneo mengine maalum.

"Zoezi la maboresho ni muhimu na lazima kwani viwanja vyote vitakaguliwa kabla ya kurejea kwa ligi na kwamba vile zitakavyoonekana kukosa sifa vitafungiwa kutumia Ligi Kuu.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FERGUSON ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inavutiwa na mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, mwenye umri wa miaka 19, lakini Brighton watadai ada ya zaidi ya pauni milioni 100 ili kumsajili. ***(Evening Standard)***

### UNITED YAMTAKA BROBBEY

KLABU ya Manchester United inafuatilia maendeleo ya mshambuliaji wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Brian Brobbey, mwenye umri wa miaka 21. ***(Mirror)***

### OSIMHEN AMFUNIKA MBAPPE

BAADHI ya viongozi wa Real Madrid wanaamini klabu hiyo inafaa kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, badala ya mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa, Kylian Mbappe (25), kutoka Paris St-Germain ***(Football Transfers)***

### DAU LA ONANA LATAJWA

EVERTON inataka pauni milioni 60 kwa kiungo wao wa kati wa kimataifa wa Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 22, lakini Arsenal italazimika kuuza mchezaji mwingine kwanza ili kumnunua nyota huyo. ***(I newspaper)***

### DIGNE ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Al-Hilal ya Saudi Arabia imefanya mawasiliano na Aston Villa kuhusu kumsajili beki wao wa pembeni wa kimataifa wa Ufaransa, Lucas Digne, mwenye umri wa miaka 30. ***(L'Equipe)***

### AGOMBEWA ENGLAND

KIUNGO wa kati wa Brentford na Nigeria, Frank Onyeka, mwenye umri wa miaka 26, anasakwa na Everton, Fulham na klabu kadhaa nje ya nchi na anatarajiwa kuruhusiwa kuondoka kwa mkopo. ***(Guardian)***

### ZIRKZEE ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inamtaka mshambuliaji wa Bologna na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### GIMENEZ KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inamfuatilia mshambuliaji wa kimataifa wa Mexico, Santiago Gimenez, mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake ni pauni milioni 30 inayotakiwa na Feyenoord. ***(Times)***

### CLARKE SOKONI EPL

WEST Ham na Crystal Palace wameonyesha nia ya kumsajili winga, Jack Clarke, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Sunderland, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa ni pauni milioni 20, huku klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur ikitarajiwa kupata asilimia 25 ya ada yoyote ya uhamisho. ***(Football London)***

### FOFONA NJIA MOJA

KLABU ya Burnley inatafuta mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 21, ambaye ameitwa kutoka kwa mkopo Union Berlin. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI: TUTAITAWALA REAL MADRID KESHO

**RIYADH,** Hispania

Hata hivyo kocha huyo afunguka ubora wa wapinzani...

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández, amesema watajaribu kuitawala Real Madrid katika mechi ya Fainali ya Supercopa ya Hispania itakayochezwa kesho baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Osasuna kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali ya pili iliyochezwa juzi Saudi Arabia.

**Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Robert Lewandowski na Lamine Yamal yaliongeza muda wa Barca kubakia mjini Riyadh na kuanzisha pambano la Clásico baada ya Madrid kuifunga Atlético Madrid katika nusu fainali nyingine hapo Jumatano.**

Mbio za bila ushindi kabla ya mwaka mpya zimeifanya Barca kupoteza pointi saba nyuma ya vinara wa LaLiga, Madrid na Girona, lakini Xavi ana matumaini makubwa kuelekea mchezo wa wikendi kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha King Saud.

"Mbinu yetu, njia yetu ya uchezaji, timu tuliyo nayo na jinsi tunavyoshindana dhidi ya Madrid," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari alipoulizwa sababu za kuamini kuwa Barca inaweza kuishinda Real.

"Mfano wa kufuata ni fainali ya mwaka jana tuliposhinda 3-1. Tulikuwa bora zaidi. Na licha ya kupoteza kwa Madrid kwenye LaLiga msimu huu, pia tulicheza vizuri hadi dakika ya 60. Tunahisi tungeweza kupata zaidi kutoka kwenye mchezo huo.

"Lazima tuchukue mpira kutoka kwa Madrid na DNA yetu inapaswa kung'aa zaidi kuliko hapo awali. Madrid wako katika hali nzuri zaidi kuliko mwaka jana, lakini tutajaribu kuwatawala na kucheza vizuri.

"Ni mazingira bora na wakati kwetu kuonesha soka letu bora zaidi. Tunaisimamia."

Lewandowski alianza kufunga dakika ya 59 dhidi ya Osasuna likiwa ni bao lake la 11 msimu huu baada ya kupokea pasi ya Ilkay Gündogan.

Wachezaji waliotokea benchi, João Félix na Lamine Yamal walicheza pamoja vizuri na kutengeneza bao la pili.

Yamal alifunga bao hilo na kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kufunga kwenye Supercopa akiwa na umri wa miaka 16 na siku 182, na Xavi alimwagia sifa zote.

"Kwa mpira, Lamine anafanya karibu kila kitu vizuri," alisema bosi huyo wa Barca.

"Hapotezi mpira na hufanya uamuzi sahihi karibu kila wakati.

"Na uzuri ni kuwa ana umri wa miaka 16 pekee. Unaona katika upande wa kimwili wa mchezo."

## HABARI MICHEZO



# MANE: SENEGAL IPO KUNDI GUMU

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Senegal, Sadio Mane, amesema wapo katika kundi gumu katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambayo inaanza leo hapa Ivory Coast.

Mane amesema timu za Gambia, Cameroon na Guinea ambazo zipo kundi moja, sio za kuzibeza kwani zinaweza kufanya lolote na kupata matokeo.

"Mchezo dhidi ya Cameroon utakuwa mgumu sana, hivyo hatuwezi kuwadharau wapinzani wetu," amesema mchezaji huyo bora mara mbili wa Afrika alipozungumza na waandishi wa habari.

"Wakati nakubaliana na hilo hakuna timu kati ya hizo ni nyepesi, tuna uwezo wa kucheza hatua ya mtoano," amesema nyota huyo wa zamani wa FC Bayern Munich na Liverpool.

Senegal iliishinda Cameroon miaka 34 iliyopita katika mchezo wa hatua ya makundi huko Algeria wakati timu hizo zilipokutana kwa mara ya kwanza katika mchezo wa Afrika.

Lakini Cameroon imekuwa ikipanda na kushuka tangu wakati huo, ikishinda Robo Fainali, baadae kishinda fainali ya mwaka 2002.

Senegal iliifunga Guinea mara mbili, lakini ilitoka suluhu kati yao katika hatua ya makundi miaka miwili iliyopita wakati ikishinda taji hilo la Afrika kwa mara ya kwanza.

# Mahrez ataja siri kushinda AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

NAHODHA wa Algeria, Riyad Mahrez, anaamini kichocheo cha kushinda michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kinatokana na maandalizi mazuri, bahati na uzoefu.

"Nchi ambayo itakuwa imefanya maandalizi mazuri na kufurahia bahati waliyokuwa nayo, basi inaweza kwenda hadi kutwaa ubingwa," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

"Uzoefu ni moja ya vitu muhimu. Mimi na wenzangu wengine waliopo katika timu ya taifa ya Algeria tunajua maana ya Kombe la Mataifa ya Afrika.

"Kuanza vizuri ni silaha kubwa na muhimu. Tuliwafunga Kenya katika mchezo wetu wa ufunguzi wa Fainali za mwaka 2019 na tulishinda taji la mashindano hayo. Tulitoka sare dhidi ya Sierra Leone miaka mitatu baadaye, lakini baadaye tulichemsha"

Mahrez, ambaye ni mzaliwa wa Ufaransa, ambaye aliondoka katika Ligi Kuu England na kutua katika Ligi Kuu ya Saudia mwaka jana, alikuwa mchezaji wa kutumainiwa katika kikosi cha Algeria nchini Misri mwaka 2019.





# *Nimerejea nyumbani - Sancho*

**DORTMUND,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Manchester United ambaye alitemwa katika kikosi, Jadon Sancho, amerejea rasmi Borussia Dortmund kwa mkopo.

Tangazo la uhamisho la Dortmund kwa Sancho liliiga taarifa ya habari ya nguli wa mpira wa kikapu, Michael Jordan maarufu "I'm back" (nimerudi) aliporejea kutoka kucheza Ligi Kuu ya Baseball na kujiunga tena na Chicago Bulls mnamo 1995.

Sancho alisajiliwa kutoka Dortmund kwa mkataba wa pauni milioni 73 mwaka 2021, lakini hajaichezea United tangu Agosti, mwaka jana kufuatia mgogoro wa hadharani na Kocha, Erik ten Hag.

Fowadi huyo amelitemwa katika kikosi cha kwanza kwa zaidi ya miezi minne baada ya kupinga hadharani sababu ya Ten Hag kumwacha wakati wa kipigo cha 3-1 kutoka kwa Arsenal Septemba 3, mwaka jana.

Katika chapisho ambalo sasa limefutwa kwenye X, ambalo zamani ilijulikana kama Twitter, Sancho alisema "sio kweli kabisa" aliachishwa kwa kutojituma kwenye mazoezi kama Ten Hag alivyodai.

Sancho ameichezea United mechi 82, akifunga mabao 12 na yuko chini ya mkataba pale Old Trafford hadi mwaka 2026.

"Nilipoingia kwenye chumba cha kubadilishia nguo leo (juzi), nilihisi kama 'nimekuja nyumbani," alisema Sancho katika taarifa yake.

"Naifahamu klabu ndani na nje, nimekuwa karibu sana na mashabiki wa hapa, na sijawahi kupoteza mawasiliano na viongozi wa hapa.

"Siwezi kusubiri kuwaona wachezaji wenzangu tena, nikitoka nje ya uwanja, kucheza soka nikiwa na tabasamu usoni, kuandaa mabao, kufunga mabao na kusaidia kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Hapo awali Ten Hag aliacha mlango wazi kwa Sancho kurejea, lakini akasisitiza lazima aombe msamaha kwanza.

"Inahusu utamaduni na kila mchezaji lazima afikie viwango fulani na ilikuwa hivyo," alisema Ten Hag Desemba, mwaka jana.

# STARS YAIPIGIA HESABU KALI MOROCCO AFCON

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Morocco, amesema wanajipanga kuhakikisha wanaanza vyema mechi yao ya kwanza ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2023), dhidi ya Morocco itakayochezwa Januari 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa San Pedro, nchini Ivory Coast.

Stars iliyoko Kundi F itashuka tena dimbani Januari 21 kucheza dhidi ya Zambia na itamaliza hatua ya makundi kwa kuvaana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

**Akizungumza na Nipashe jana, Morocco, alisema hali ya hewa ni nzuri na haithiri programu za maandalizi ya michuano hiyo na tayari wamesahihisha makosa yaliyojitokeza katika mechi ya kirafiki ya kimataifa waliyocheza dhidi ya Misri.**

Kocha huyo alisema tayari wameweka mipango na mikakati sawa kuelekea mchezo huo wa kwanza ambao wanaamini utakuwa na ushindani kwa sababu timu hizo mbili ziliwahi kukutana hivi karibuni na Tanzania kufungwa mabao 2-0.

"Tumefanyia kazi mapungufu ya kikosi chetu na tunajua utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa sana kwa sababu Morocco tumeshawahi kucheza nao hivi karibuni, kila mmoja anamfahamu mwenzake lakini tumeandaa kikosi vyema, wachezaji wako tayari kwa mapambano," alisema Morocco.

Naye beki wa kati wa timu hiyo, Dickson Job, alisema wamefanya mazoezi vizuri na wachezaji wote wako tayari kuanza fainali hizo na sasa akili yote inaisubiri Morocco, mechi ambayo itawapa dira la wapi wanaelekea katika michuano hiyo.

Job alisema wanaifahamu vizuri Morocco kwa sababu walicheza nayo na wanaamini wanayo nafasi ya kuvuka hatua ya makundi na kusonga mbele.

"Kwa sasa cha muhimu ni kuitazama Morocco, tuko tayari kupambana, tuko tayari kuhakikisha tunaipeperusha vyema bendera ya Tanzania, ninaimani tukipambana na kujitoa kwa asilimia 100 tunavuka hatua ya makundi," beki huyo alisema.

Aliongeza kila timu imejiandaa vizuri na michuano hiyo na makundi yote ni magumu.



Wachezaji wa timu ya Soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva (kushoto) na Mbwana Samatta (kulia), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi yao ya kwanza dhidi ya Morocco katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), itakayofanyika Januari 17, mwaka huu, nchini Ivory Coast. **PICHA:TFF**

# Simba, Mlandege fainali ya kiumeni

INATOKA UKURASA 24

Aliongeza uongozi umeamua kumwachia majukumu yake Benchikha kwa kutoingilia mambo yake hasa katika kuhakikisha Simba inakuwa imara na wachezaji kujutuma kwa kupambana.

"Ni kweli kocha Benchikha ni mkali na huwa anahitaji mchezaji kufuata maelekezo yake kwa asilimia 100, ndio maana sasa hivi tunaona jinsi ya wachezaji wanavyojituma, wanapambana uwanjani tofauti na ilivyo awali," meneja huyo alisema.

Benchikha amewaambia wachezaji wake anataka ushindi ndani ya dakika 90, badala ya kusubiri penalti, hivyo wanatakiwa kutumia vizuri kila nafasi itakayopatikana.

Benchikha alisema anafahamu fainali haitakuwa rahisi kwa sababu siku zote huwa ni mechi ya mbinu zaidi kuliko burudani na ufundi na anatarajia upinzani kama walioupata kutoka kwa Singida Fountain Gate.

"Mechi itakuwa ngumu, nimewaambia wachezaji wangu kuwa makini, kutofanya makosa madogo madogo ambayo yatatugharimu, lakini pia kutumia nafasi chache tunazozipata kwa ajili ya 'kuua' mechi, sihitaji kwenda mpaka katika mikwaju ya penalti, nimewaambia kama watacheza kwa maelekezo na kufuata kile ambacho nimewaagiza tunaweza kuimaliza kwa dakika 90 tu," alisema kocha huyo raia wa Algeria.

Ofisa Habari wa Mlandege, Ally Mohamed, alisema wachezaji wao wamewaahidi kuwapa donge nono endapo wataibuka na ushindi na hiyo ni kawaida yao, hata mwaka jana walifanya hivyo.

"Klabu imeweka dau nono kwa wachezaji wake iwapo watafanikiwa kuifunga Simba na kuubakiza ubingwa wa michuano ya Mapinduzi. huu umekuwa ni utaratibu wetu wa kawaida wachezaji kupata zawadi kutoka kwa viongozi timu inapofanya vizuri na hata mwaka jana ilikuwa hivi hivi, kwa hiyo watu wasidhani ni kwa sababu tunacheza dhidi ya Simba," alisema Mohamed.

## Watano wakosa penalti Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya penalti 19 zimetolewa mpaka kufikia raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku 14 zikiwekwa wavuni na tano zikiota mbawa baada ya makipa kuokoa au wachezaji wenyewe kukosa.

Kwa mujibu wa takwimu zetu za Bodi ya Ligi zilizotolewa jana, penalti hizo zimekoswa na wachezaji watano tofauti.

Wachezaji waliokosa penalti ni Bruno Gomes wa Singida Fountain Gate, Erick Mukombozi (Namungo FC), Elius Maguri (Geita Gold), Enock Mayala (Coastal Union) na Obrey Chirwa wa Kagera Sugar.

Takwimu za dawati la michezo la Nipashe zinaonyesha Maguri alikosa penalti katika mechi ambayo Geita Gold ilipata kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa KMC wakati Chirwa akikosa katika mechi ambayo Kagera Sugar ilichapwa magoli 4-0 na Azam FC huku Mulokozi penalti yake ikiota mbawa katika mechi ambayo Namungo ikicheza dhidi ya Ihefu na kupata ushindi wa mabao 2-0.

Mayala wa Coastal alikosa penalti timu yake ilipocheza dhidi ya Mashujaa, lakini waliondoka na ushindi wa mabao 2-0.

Katika mabao 14 ambayo yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu, Saido Ntibazonkiza anaongoza kwa kufunga mabao mengi ya penalti akiwa nayo matatu mpaka sasa.

## Gamondi afunguka straika anayemtaka

INATOKA UKURASA 24

na Aziz Ki," kilisema chanzo kutoka klabuni hapo.

Yanga inatajwa ilianza mazungumzo na straka, Glody Kilangalanga, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), anayeichezea Bisha FC ya Saudia Arabia, lakini mazungumzo yanadaiwa kusuasua kutokana na sababu mbalimbali.

Nyota huyo alitajwa kuna kuchukua nafasi ya Hafidh Konkoni, ambaye hajacheza mechi yoyote ya kimataifa inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Pamoja na kucheza mechi mbalimbali za Ligi Kuu Bara na kufanya vyema kwenye baadhi ya mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, bado wanachama na mashabiki wa Yanga wamekuwa wakilalamika timu yao kutokuwa na straika mwenye makali kama Fiston Mayele, aliyeuzwa katika klabu ya Pyramids ya Misri.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA huku msimu uliopita ikicheza fainali ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Michezo
Jumamosi Januari 13, 2024
Nipashe



**Xavi: Tutaitawala Real kesho** UKURASA 21

# Simba, Mlandege fainali ya kiumeni

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba inatarajia kukutana na Mlandege katika fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi umefunguka kuhusu tetesi za mshambuliaji wao, Kibu Denis, kutakiwa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

**Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Mamelodi Sundowns imewasilisha rasmi ofa kwa Simba ya kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo ambaye kwa sasa yuko katika kikosi cha Timu ya Taifa kilichoko kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini, Ivory Coast.**

Chanzo chetu kinasema hii ni mara ya pili kwa Mamelodi Sundowns kutuma ofa kuhusiana na Kibu lakini uongozi wa Simba ukikaa kimya kuhusiana na maombi hayo.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema katika meza ya klabu hiyo hakuna ofa kuhusu Kibu au mchezaji mwingine anayetakiwa na wao kwa sasa wanafikiria kuimarisha kikosi chao.

Ahmed alisema Simba inahitaji kukijenga imara kikosi chao ili kuongeza ushindani na kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao.

Alisema mashabiki wa Simba wasiwe na wasowaso juu ya taarifa hizo kwa sababu hakuna taarifa rasmi waliyopokea ya kutakiwa kwa Kibu au Willy Onana ambaye naye anahusishwa kuwindwa na JS Kabylie ya Algeria.

"Hawa wachezaji wako katika mipango ya kocha wetu (Abdelhak Benchikha), kwa sasa tunahitaji kuboresha kikosi cha timu kama ulivyoona tumeshatambulisha wachezaji watatu akiwamo, Salehe Karabaka, Babacar Sarr na Ladack Chasambi, na hivi karibuni tutamtambulisha nyota mwingine.

Tunahitaji kuongeza mtu, hiki kipindi sio cha kuondoa wachezaji muhimu kwa kuuza kwa sababu ni muda wa kuboresha kama ilivyo kwetu tunaboresha kulingana na nafasi zilizopendekezwa," alisema Ahmed.

ENDELEA UKURASA 23

## ●●● Mamelodi Sundowns yarejea tena Msimbazi ikimtaka Kibu...



Fabrice Ngoma



Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi

# Gamondi afunguka straika anayemtaka

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anahitaji kupata straika mpya mwenye viwango vya juu na endapo atakosekana, yuko tayari kutosajili nyota mpya.

Taarifa kutoka ndani ya Yanga zinasema Gamondi ameweka wazi yuko tayari kuwatumia wachezaji waliopo na kusubiri wakati wa dirisha kubwa la usajili ili kupata mchezaji mwenye kiwango sahihi anachohitaji.

"Kocha amefikia uamuzi huo baada ya kuona viongozi wanahaha kusaka straika wa viwango vya juu, amesema kama ni ngumu kupata straika wa maana, ataendelea kuwatumia viungo washambuliaji walioko (Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli na Stephane Aziz Ki), kupachika mabao kwa sababu bado wana uwezo mkubwa wa kufanya hivyo na timu ikaendelea kutisha," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza pia Gamondi amefikia uamuzi huo baada ya kubaini straika mpya atakayetua atahitaji muda wa kuzoeana na wenzake jambo ambalo linaweza kuwagharimu wakati timu iko katika mbio za kutetea ubingwa na kufanya vyema kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kocha amewaambia kama hatopatikana straika wa viwango vya juu basi hakuna haja ya kusajili mtu ambaye ligi ikiisha atawasumbua kuvunja mkataba na kumlipa, waache tu ataendelea na Kennedy Musonda na Clement Mzize, lakini msingi wake mkubwa itakuwa ni Pacoma, Mazi

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >